

**Diamond** kuzoa bilioni 11.5

UKURASA 20



**Zidane** ana matumaini Messi hataondoka Barcelona

UKURASA 21

**MAISHA**

APRILI 11, 2021 Nipashe — Baba, Mama na Mwana — *Jumapili*



Ukurasa 10

**Anatembea kike, nani wa kulaumiwa?**



Ukurasa 15

**MAISHA NI NYUMBA**

Fanya haya kupendezesha mandhari ya nyumba yako



**HARUSI**

Ukurasa 12


# Nipashe Jumapili

Jumapili Aprili 11, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0580547

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




**USIJIKONDESHE**

**Hipsi hujengwa kwa mazoezi**

Ukurasa 14

UKURASA 9

# Prof. Assad apasua jipu



• **Aanika** viongozi wengi hawana uwezo, wasaka tonge, CAG afukua madudu zaidi TPA, Ngorongoro...*Ukurasa 2&3*

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

**AKATWA KICHWA KISHA WAUAJI KUONDOKA NACHO**

MKAZI wa kijiji cha Janda, Buhigwe mkoani Kigoma, Shinje Mugalama, ameuawa kikatili na watu wasiojulikana kwa...

## Kenyatta amwalika Rais Samia Kenya

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan, akipokea barua yenye ujumbe maalum kutoka kwa Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta, iliyowasilishwa kwake na Dk. Amina Mohammed ambaye ni mjumbe maalum wa Rais Kenyatta, Ikulu Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play — Download on the App Store


UKURASA 2

## Bosi Bodi Utalii atumbuliwa

**MICHEZO** — **CHAMA: NGUVU ZOTE ROBO FAINALI** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Kenyatta amwalika Rais Samia Kenya

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kukuza uhusiano na ushirikiano baina ya Tanzania na Kenya, Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta, amemwalika Rais Samia Suluhu Hassan, kufanya ziara rasmi nchini humo.

Vilevile, Rais Kenyatta amemhakikishia Rais Samia kuwa Kenya iko tayari wakati wote kushirikiana na Tanzania kwa kuendeleza na kukuza zaidi ushirikiano kati ya nchi hizo.

Hayo yamebanishwa jana wakati Rais Samia alipopokea ujumbe maalum kutoka kwa Rais Kenyatta, uliowasilishwa na Waziri wa Michezo, Utamaduni na Urithi wa Kenya, Balozi Dk. Amina Mohamed.

Taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu, Gerson Msigwa, ilisema pamoja na kupokea ujumbe huo, Ikulu jijini Dar es Salaam, Rais Samia alifanya mazungumzo na Balozi Amina kuhusiana na dhamira ya Tanzania na Kenya kuendeleza na kukuza zaidi uhusiano, ushirikiano katika nyanja mbalimbali hususani kiuchumi na kijamii.

"Rais Samia amemhakikishia Rais Kenyatta kuwa serikali anayoiongoza iko tayari kuendeleza mambo mazuri yote yaliyokuwa yakifanywa na mtangulizi wake, Hayati Dk. John Magufuli, na kutatua changamoto kati ya Tanzania na Kenya kwa kuwa nchi hizi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ni ndugu, majirani na marafiki wa kihistoria," ilieleza taarifa hiyo.

Vilevile, Rais Samia aliwataka mawaziri na wataalamu wa Tanzania na Kenya wanaounda Kamati ya Ushirikiano wa Pamoja (JPC) ambao hawajakutana tangu mwaka 2016 kukutana mara moja ili kufanyia kazi masuala mbalimbali ya kuimarisha uhusiano.

Katika mazungumzo hayo, Balozi Amina aliongozana na Balozi wa Kenya hapa nchini, Dan Kazungu.




Mafundi wakiendelea na ujenzi wa kingo na upanuzi wa Mto Ng'ombe, eneo la Ubungo Maji, Manispaa ya Kinondoni, mkoani Dar es Salaam jana, ambapo awali ulikuwa ukielemewa na mafuriko nyakati za mvua na maji kuleta madhara kwenye makazi ya watu. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Prof. Assad apasua jipu

**Na Mwandishi Wetu**

ALIYEKUWA Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, amesema hatua ya mawaziri kufanya operesheni maeneo mbalimbali wanakosea bali wajue wao ni wa kupanga mikakati na sera.

Amesema kwa sasa idadi kubwa ya watu wanataka uteuzi wa uwaziri ili kufanya biashara na si kuwatumika wananchi.

Alitoa kauli hiyo jana Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa mfululizo wa midahalo kwa umma ulioandaliwa na Chuo Kikuu cha Kiislamu Morogoro (MUM).

Sambamba na hilo, alisema viongozi wengi serikalini na taasisi za umma hawana uwezo kiutendaji, hivyo kuna umuhimu wa kuanza upya ili kuwezesha maendeleo ya taifa kupatikana.

"Kupanga mikakati na sera ndiyo kazi ya waziri na si kwenda vijijini kufanya operesheni za kutatua matatizo," alisema Prof. Assad.

Jana, akiwa katika mdahalo huo, alitoa mtazamo wake kwa kueleza kuwa viongozi wengi serikalini si wazuri na wanapaswa kupumzishwa ili mambo yaende vizuri.

Prof. Assad alisema kutokana na tatizo hilo, kuna haja ya kuanza na safu mpya ya viongozi serikalini kwa madai waliopo wengi hawana uwezo mzuri kiutendaji.

"Tatizo ni kwamba watu wote wamekuwa waoga, imefika mahali watu wengine wananyamaza tu, ndiyo maana nasema tuanze upya tuanze na hao wachache ambao wanakwenda vizuri.

"Hilo pia ni somo kwamba ambao nao baadaye watakuwa wa ovyo ovyo. Dawa yao ni hiyo ya kuwaweka kando na kuanza upya," alisema.

Katika mkutano huo, Prof. Assad alisema kuna watu waliunga mkono utawala uliopita na sasa wanaunga tena vitu ambavyo haviendani na kueleza watu wa aina hiyo ni wasaka fursa ambao hawasaidii chochote.

Akizungumzia mradi wa Bandari ya Bagamoyo, Prof. Assad alisema anashindwa kusema kama ni mzuri au la kwa sababu nyaraka zake bado hajaziona.

Hata hivyo, alisema ipo haja ya serikali kutoa nyaraka za mradi huo na kuziweka hadharani ili wananchi waangalie na kutoa maoni yao na kuona kama ni wa faida au hasara.

Kuhusu upigaji kura, Profesa Assad alisema mfumo wa kupiga kura kwa makaratasi si rafiki kwake na kwamba hatashiriki katika upigaji kura hadi pale mfumo wa dijitali utakapotumika.

Prof. Assad alisema: "Nataka nikipiga kura hapa nione moja kwa moja kura yangu ilivyohesabiwa".

Naye Makamu Mkuu wa MUM, Prof. Hamza Njozi, akizungumza katika mdahalo huo, alisema jana ilikuwa mwanzo wa kufanyika kwa mdahalo huo na kwamba wanajiandaa kufanya kila mwezi.

Alisema kila mwezi mdahalo huo utawajumuisha wasomi ambao watakuwa wanachambua baadhi ya masuala na kwamba mada zitakuwa tofauti.

# Bosi Bodi ya Utalii atumbuliwa

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, jana amemsimamisha kazi Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Devotha Mdachi, kupisha uchunguzi kutokana na tuhuma za ubadhirifu wa fedha.

Waziri Ndumbaro aliagiza jana kusimamishwa kwa mkurugenzi huyo huku akikisitiza kuwa uchunguzi huo hauhusiani na Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) iliyowasilishwa wiki hii bungeni jijini Dodoma.

Alisema nafasi hiyo iliyoachwa wazi, itakaimiwa na Betrita James ambaye ni Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhifadhi TANAPA.

Waziri Ndumbaro alisema hawawezi kumchunguza mtu akiwa kakalia kiti hicho hicho.

Mdachi aliteuliwa na Rais wa Nne wa Tanzania, Jakaya Kikwete, kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa TTC Oktoba 23, 2015.

Aliajiriwa TTB mwaka 1994, akiwa Ofisa Habari masuala ya Utalii katika tawi la Arusha na baadaye mwaka 1998, alihamishiwa Dar es Salaam katika Kituo cha Habari za Utalii ambako alipandishwa kuwa ofisa mwandamizi na ofisa habari za utalii mkuu.

Mwaka 2010, alipandishwa kuwa Ofisa Masoko Mkuu wa bodi hiyo kabla ya kuteuliwa kushika wadhifa wa sasa kabla ya kusimamishwa.

## HABARI KITAIFA

# Uhaba wa watumishi washtua

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), amebaini uhaba mkubwa wa watumishi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa unaosababisha kutokuwa na ufanisi katika utendaji.

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2019/20 iliyowasilishwa bungeni Alhamisi, CAG Charles Kichere, anasema mapitio ya ikama za Mamlaka 123 za Serikali za Mitaa yalibaini idadi halisi ya watumishi waliopo ni 233,281 kulinganishwa na mahitaji ya watumishi 353,034 na kusababisha upungufu wa watumishi 119,753 (asilimia 34).

"Upungufu huu unaathiri utendaji wa jumla wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ikiwa pamoja na utoaji wa huduma duni, mrundikano wa majukumu na kupunguza morali ya kazi kwa watumishi waliopo.

"Pia, nilibaini kuwa malengo ya serikali ya kutekeleza miradi mingi kwa kutumia utaratibu wa nguvukazi ambayo inahitaji wataalamu wa kutosha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa yanaweza yasifikiwe kwa mafanikio kutokana na upungufu huu wa watumishi.

"Vivyo hivyo, uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya msingi na sekondari pamoja na huduma bora za afya katika ngazi za vijiji na kata umekuwa ukiongezeka kila mwaka, ambao pia unahitaji walimu na wahudumu zaidi wa afya," anasema.

CAG pia anabainisha kuwapo kwa malimbikizo ya stahiki za watumishi kiasi cha Sh. bilioni 27.84; kutorejeshwa kwa mishahara isiyolipwa kwa sababu mbalimbali kiasi cha Sh. milioni 82.581; na watumishi 7,992 kutoka katika halmashauri 14 kuchelewa kupandishwa vyeo ingawa walikuwa na vigezo.

"Vilevile, niliendelea kubaini udhaifu wa baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kuzingatia sheria, kanuni na maelekezo yanayohusiana na usimamizi wa rasilimali-watu na mishahara," anabainisha.

CAG anatoa wito kwa Menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa, Idara ya Utumishi na Ofisi ya Rais - TAMISEMI kuwa na utaratibu ambao utahakikisha upatikanaji wa fedha za kuajiri watumishi ili kujaza nafasi zilizo wazi.

Katika hatua nyingine, CAG anatoa hadhari kuhusu watumishi kutopandishwa madaraja, akionya kuwa ni kinyume cha Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za Mwaka 2009.

"Nilipitia mafaili ya watumishi pamoja na Mfumo wa LAWSON wenye taarifa mbalimbali za watumishi na kubaini kuwa, watumishi 7,992 katika Mamlaka 14 za Serikali za Mitaa hawakupandishwa madaraja ingawa walikuwa na sifa kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma," anabainisha.



Mwendesha pikipiki akiwa amebeba mzigo mkubwa wa mkaa na abiria akining'inia katika eneo la Msongola, jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Madudu zaidi yafukuliwa TPC

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), amebaini miamala 737 iliyotumika kufanya ubadhirifu wa fedha katika Mamlaka ya Bandari (TPA).

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2019/20, CAG Charles Kichere, anabainisha kuwa alibaini vitendo hivyo vya ubadhirifu katika Bandari ya Mwanza na Bandari ya Kigoma.

Anabainisha kuwa katika Bandari ya Mwanza, Sh. bilioni 3.27 zilitolewa katika akaunti ya benki ya TPA iliyoko CRDB kupitia miamala 737.

Anasema kuwa malipo hayo hayakuwa na hati za malipo na matumizi ya fedha hizo hayakuonyeshwa katika taarifa za fedha.

**HUNDI 30 ZATUMIKA**

"Katika Bandari ya Kigoma, Sh. milioni 655.9 zilitolewa kutoka benki kwa kutumia hundi 30 bila kuwa na hati za malipo kuthibitisha malipo yaliyofanywa, na hundi hazikusajiliwa kwenye daftari la udhibiti wa hundi, na vipande vitano vya hundi havijaonekana katika daftari la udhibiti wala katika taarifa za benki.

"Nyaraka kama vitabu vya hundi, hati za uhamishaji fedha na taarifa za bodi ya zabuni hazikutolewa kwa uchunguzi zaidi. Pia, katika Bandari ya Kigoma, nilibaini ukosefu wa ripoti za mapato za kila siku ili kuhakiki ripoti za mapato ya kila mwezi kwa kipindi cha miezi saba.

"Ukamilifu na usahihi wa mapato yaliyokusanywa hayawezi kuhakikiwa kwa sababu ya kukosekana kwa hati za msingi za mapato," anabainisha CAG.

Anasema hali hiyo inasababisha upotevu wa fedha za serikali ikiwa fedha hazitarejeshwa. Hivyo, anapendekeza TPA kwa kushirikiana na vyombo vya usalama, ihakikishe fedha zinapatikana na hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya watu waliohusika.

# Milioni 700/- ununuzi basi la hifadhi zapotea

**Na Sanula Athanas, DODOMA**

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), amebaini hatari ya kupotea kwa Sh. milioni 714.12 zilizotolewa na serikali kwa ajili ya ununuzi wa basi katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA).

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2019/20 ilioyowasilishwa bungeni jijini Dodoma Alhamisi, CAG Charles Kichere, anasema NCAA ilipewa kibali na Ofisi ya Waziri Mkuu kununua magari 10.

Anafafanua kuwa moja ya magari hayo ni basi aina ya 'Mercedes Benz four wheel drive' ambalo lilihitajika kwa shughuli za utalii ndani ya kreta na maeneo mengine ya Hifadhi ya Ngorongoro.

"Baada ya Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini (GPSA) kupata vigezo vya basi lililohitajika kutoka TEMESA kupitia barua zenye kumbukumbu Na. TEM/AR/03028 na TEM/AR/030530/VOL.III/79, NCAA walilipa GPSA kiasi cha Sh. milioni 714.12 (Dola za Marekani 311,605.18) ili inunue gari mpya aina ya 'Mercedes Benz four wheel drive' lenye uwezo wa kubeba abiria 40 hadi 47. 91.

"Wakati wa ukaguzi, nilibaini kuwa GPSA haikuzingatia vigezo ilivyopewa kwa ajili ya ununuzi wa basi, badala yake ilinunua gari la 'two wheel drive' ambalo lilikuwa limeshatembea kilomita 1,752 badala ya kilomita sifuri.

"Basi hilo halikidhi sera za Ngorongoro ya kutumia 'four wheel drive' na sera ya serikali ya kununua magari yenye kilomita sifuri.

"NCAA walilirudisha basi hilo kwa GPSA na tayari limesajiliwa kwa jina la GPSA kwa kuwa haliwezi kutumika kwa shughuli za utalii maeneo ya kreta.

"Kwa kuwa GPSA haijatoa majibu yoyote kuhusu basi hilo, nina shaka kwamba NCAA inaweza kutorudishiwa basi au malipo yake kwa GPSA, hivyo fedha hizo zinaweza kupotea bila faida yoyote kwa NCAA," anaonya.

Katika ripoti yake hiyo, CAG anapendekeza NCAA katika kufuatilia fedha zao, iishirikishe Wizara ya Kazi, Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Maliasili na Utalii ili waingilie kati suala hili.

**MNADA WA HADHARA**

Kwa idhini tuliyopewa na TUJIJENGE TANZANIA LTD, SEPCO DEBT COLLECTION & AUCTIONEERING CO. LTD tutauza kwa mnada wa hadhara, mali ya mdaiwa Sugu Ndugu Amina Martin Bagule. Shamba lenye nyumba aliyoweka dhamana ya mkopo iliyopo Kimara –Mtaa wa King'azi kwa mujibu wa sheria. Mnada utafanyika tarehe 17/04/2021 kuanzia saa nne (4) asubuhi mara baada ya gari la matangazo kupita sehemu mali husika ilipo.

Lengo ni kufidia/ kupunguza deni la mkopo analodaiwa. Mnada utafanyika Tarehe 17/04/2021, mahali dhamana ilipo. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14 akishindwa kulipa 25% hairudishwi.

Gharama za kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga: 0715683777/ 0712670704/ 0713052578**
**Email: info@sepcoauctioneering.co.tz**

## TAKUKURU yaokoa mamilioni ya wastaafu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Dodoma, ndani ya miezi sita, imeokoa Sh. milioni 704.1 za malipo ya tozo za halmashauri zilizokuwa mikononi mwa watendaji.

Mkuu wa TAKUKURU mkoani hapa, Sosthenes Kibwengo, alisema kati fedha hizo, Sh. milioni 214.1 ni za watumishi waajiriwa na wastaafu wa sekta binafsi ambao makato yao hayakuwasilishwa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) kwa wakati na kuwaletea usumbufu mkubwa.

"Baadhi ya waajiriwa wa sekta binafsi hawawasilishi makato yote, hivyo kwa kushirikiana na NSSF mkoani Dodoma wamedhibiti kiasi hicho cha fedha kutoka kwa waajiri 30," alisema.

Alifafanua kuwa Sh. milioni 27 kati ya fedha zimetokana na ufuatialiaji wa miradi miwili ya maji ambayo ilibainika kuwa na malipo batili yaliyofanywa na makandarasi wa vijiji vya Goima wilayani Chemba na Mundemu wilayani Bahi ilihali kazi zilizoanishwa hazikufanyika.

Kibwengo alisema ukaguzi uliofanywa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za serikali (CAG), ulithibitisha upungufu huo na kuelekeza pamoja na hatua zingine, makandarasi na wasimamizi wa miradi hiyo warejeshe fedha zilizolipwa kinyume cha utaratibu.

Katika hatua nyingine, Kibwengo alisema TAKUKURU inamshikilia mfanyabiashara Luka Nkini (38) mkazi wa Airport jijini Dodoma, kwa tuhuma za kujipatia zaidi ya Sh. milioni 105 kwa manufaa kinyume na Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa akijifanya mganga na mjukuu wa Babu Mitimingi wa Kigoma.

Kibwengo alisema Nkini amekuwa akijipatia fedha na mali zingine kutoka kwa watu mbalimbali ikiwamo malipo kutoka kwa kinamama 10 ambao amekuwa akiwadanganya ya kuwa kiasi cha fedha ambacho watatoa kitazidi mara mbili huku akiwapa sharti la kufanya ngono na baadhi yao.

Alisema mtuhumiwa huyo amekuwa akifanya uhalifu huo katika mikoa ya Dodoma, Arusha na Kilimanjaro na amejipatia viwanja viwili, mashamba mawili, vifaa vya kielektroniki na samani.

Kwa mujibu wa Kibwengo, baada ya kukamatwa, Nkini alikiri makosa na kuwataja wenzake ambao anashirikiana nao katika kufanya uhalifu huo ambao ni Hussein Mvungi (44) mkazi wa Himo Kilimanjaro ambaye ameshakamatwa na Gabriel Munuo, mkazi wa Sanya Juu Siha.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akikagua ujenzi wa mradi wa Bwawa la kuzalisha umeme la Nyerere, wilayani Rufiji, mkoani Pwani jana. Kushoto ni Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato. **PICHA: OWM**

## Majaliwa atangaza neema watumiaji umeme

**Na Beatrice Shayo, Rufiji**

WAZIRI Mkuu Kassimu Majaliwa, amesema kukamilika kwa ujenzi wa bwawa la kuzalisha umeme wa maji la Julius Nyerere (JNHPP) kwenye Mto Rufiji, kutashusha gharama za nishati hiyo hadi Sh. 36 kwa uniti moja ifikapo mwakani.

Kadhalika, Majaliwa amesema anayebeza mradi huo apatiwe fursa ya kutembelea ili aone maendeleo makubwa yaliyofanyika badala ya kutoa taarifa ya upotoshaji kuwa mradi hauna maslahi.

Waziri Mkuu aliyasema hayo jana alipofanya ziara katika mradi huo ambao unagharimu Sh. Trilioni 6.5 na utakamilika na kukabidhiwa kwa serikali Juni, mwakani.

Alisema umeme wa maji una faida nyingi katika nchi kuliko vyanzo vingine vinavyozalisha nishati ya umeme.

Majaliwa alisema mradi huo utazalisha megawati 2,115, hivyo kutakuwa na ongezeko la umeme na mwingine kuuza nje ya nchi.

"Umeme wa maji gharama zake si zaidi ya Sh. 36 hata kama kutakuwa na mabadiliko ya bei haitazidi Sh. 50 lakini umeme wa gesi Sh. 147 kwa uniti lakini umeme ambao tunautumia huu wa mafuta gharama zake ni kubwa kuanzia Sh. 440 hadi 600 ni gharama kubwa kwa uniti moja," alisema

Majaliwa alisema kwa uchunguzi walioufanya, viongozi wamegundua nchi ambazo wananchi wake wanatumia umeme wa maji, wanapata faida kubwa kwa kununua umeme kwa gharama ndogo na Tanzania ndiko inakoelekea kununua nishati hiyo kwa Sh 36.

"Faida nyingine kutakuwa na umeme wa uhakika na serikali itapata faida kwa kuuza umeme nje ya nchi na bwawa hii ni la nne kwa ukubwa Afrika tutawauzia umeme majirani zetu maana wana uhitaji," alisema.

Waziri Mkuu alisema mradi unaendelea vizuri katika maeneo yote sita aliyoyatembelea na makandarasi wa ujenzi huo wanazingatia viwango vya ubora na hadi sasa umekamilika kwa asilimilia 47.

"Kwa maeneo nyeti ya mradi yamekamilika kwa kiwango cha asilimia 47 na kipindi kilichobaki kinaweza kufika Juni, 2022. Ninaamini watakamilisha ndani ya muda," alisema.

"Nimepata nafasi ya kutembelea eneo linalochemsha maji ambalo ni eneo la maporomoko ya maji kutakuwa na mitambo ya uzalishalishaji umeme ambayo kazi nzuri nimeona iliendelea pia nimeona daraja litakalotuunganisha pande mbili ujenzi wake unaendelea na wataalamu wetu wametuambia viwango vimezingatiwa," aliongeza.

Waziri Mkuu alisema baada ya bunge la bajeti, atarudi kufuatilia mradi huo na kutoa fursa kwa wabunge na wananchi kuutembelea ili wajionee maendeleo yaliyofikiwa.

"Kwa wale wasiopenda maendeleo kuna upotoshaji katika wa mradi huu, mara mradi hauendi, mara ujenzi hautakamilika mara ujenzi hauna maslahi kwa nchi, naomba utoe fursa kwa wananchi wachache waje kujionea huu mradi wawe mabalozi wa Watanzania wengine," alisema Majaliwa.

Mshauri wa mradi, John Mageni, alipohojiwa kuhusiana na kutumia upembuzi yakinifu wa mwaka 1970 katika mradi huo, alisema taarifa hizo si za kweli wamehuisha kutumia ya mwaka 2017 ambayo mkandarasi ameukubali na mradi unafanyika kwa viwango vya ubora.

## Auawa kwa kukatwa kichwa kisha wauaji kuondoka nacho

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

MKAZI wa kijiji cha Janda, Buhigwe mkoani Kigoma, Shinje Mugalama, ameuawa kikatili na watu wasiojulikana kwa kukatwa shingo na kutenganishwa kichwa na kiwiliwili kisha watu hao kutokomea kusikojulikana na kichwa hicho.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kigoma, Kamishna Msaidizi, (ACP) James Manyama, alisema alhamisi iliyopita, Mugalama ambaye hakuwa na makazi ya kudumu, alifika nyumbani kwa Juma Zegeri kuomba hifadhi baada ya kudai kuna watu (ambao hakuwataja majina) amegombana nao na wanamfuatilia.

Manyama alisema mtu huyo alipokewa na kupewa sehemu ya kulala ambayo ni jiko lililokuwa pembeni ya nyumba kubwa ya Zegeri na usiku wa kuamkia juzi, alivamiwa na watu wasiojulikana ambao walimkata kichwa na kutokomea nacho.

Kutokana na tukio hilo, alisema Jeshi la Polisi linawashikilia watu wawili baada ya kuendesha opereshani ya kuwatafuta huku likiendelea kuwatafuta wengine zaidi wanaodaiwa kuhusika na tukio hilo.

"Nichukue fursa hii kuwataka watu wa Kigoma kutojihusisha na vitendo vya uhalifu na kujichukulia sheria mkononi," alisema.

Kwa mujibu wa kamanda manyama, mwili wa Marehemu umeshafanyiwa uchunguzi na kukabidhiwa kwa ndugu ili waendelee na taratibu za mazishi huku taratibu za kukamilisha upelelezi na kuwafikisha mahakamani wanaodaiwa kuhusika na tukio hilo zikiendelea.

TANGAZO

# TATEPA PUBLIC LIMITED COMPANY

## RESULTS FOR THE THE YEAR ENDED 30 SEPTEMBER 2020

### STATEMENTS OF PROFIT OR LOSS ACCOUNTS AND OTHER COMPREHENSIVE INCOME

For the period ended 30 September 2020

| | GROUP | | COMPANY | |
|---|---|---|---|---|
| | 30 Sept 2020 Audited Tzs' 000' | 30-Sept-2019 Audited Tzs' 000' | 30 Sept 2020 Audited Tzs' 000' | 30-Sept-2019 Audited Tzs' 000' |
| **Revenue** | 22,873,346 | 23,570,168 | - | - |
| Cost of sales | (16,984,015) | (22,172,207) | - | - |
| **Gross profit** | **5,889,331** | **1,397,961** | **-** | **-** |
| Other income | 284,368 | 314,488 | 190,906 | 141,896 |
| Selling and marketing costs | (2,444,907) | (2,033,077) | - | - |
| Administrative expenses | (5,731,576) | (3,980,151) | (1,882,281) | (1,025,714) |
| Grant amortisation | 20,279 | 20,279 | - | - |
| Fair value (loss)/gain on embedded derivative | (457,647) | (178,907) | (457,647) | (178,907) |
| **Operating profit / (loss)** | **(2,440,152)** | **(4,459,407)** | **(2,149,022)** | **(1,062,725)** |
| Finance Costs - net | (1,643,167) | (1,180,983) | 563,964 | 347,422 |
| Exchange profit/(Loss) & Finance income | | | | |
| Profit /(loss) before income tax | (4,083,319) | (5,640,390) | (1,585,058) | (715,303) |
| Income tax credits /(expenses) | (101,479) | (1,998,790) | - | - |
| **Profit for the year** | **(4,184,798)** | **(7,639,181)** | **(1,585,058)** | **(715,303)** |
| Profit / (loss) on disposal of subsidiary KTPC | - | 1,944,400 | - | (5,501,827) |
| Statement of Comprehensive income | | | | |
| Profit /(loss) for the year | (4,184,798) | (5,694,781) | (1,585,058) | (6,217,130) |
| Profit / (loss) for the year | (4,184,798) | (5,694,781) | (1,585,058) | (6,217,130) |
| **(Loss)/ profit attributable to:** | | | | |
| Owners of the parent | (3,240,092) | (2,917,979) | (1,585,058) | (6,217,130) |
| Non-controlling interests | (944,707) | (2,776,802) | 0 | 0 |
| | **(4,184,799)** | **(5,694,781)** | **(1,585,058)** | **(6,217,130)** |
| **Other Comprehensive Income:** | | | | |
| Item that will not be seclassified to profit or loss: | | | | |
| - Gain on revaluation of biological assets | - | | | |
| - Actuarial gain / (loss): net of tax | | | | |
| **Total comprehensive income/(loss) for the year** | **(4,184,799)** | **(5,694,781)** | **(1,585,058)** | **(6,217,130)** |
| **(Loss)/ profit attributable to:** | | | | |
| Owners of the parent | (3,240,092) | (2,917,979) | | |
| Non-controlling interests | (944,707) | (2,776,802) | | |
| | **(4,184,799)** | **(5,694,781)** | | |
| **Dividend:** | | | | |
| Proposed final dividend for the year | | | | |
| Earnings per share attributable to the equity holders of the Company during the year (expressed in Tsh per share) | | | | |
| Basic earnings per share | (173.66) | (156.40) | | |
| Diluted earnings per share | (36.20) | (34.89) | | |

### STATEMENT OF FINANCIAL POSITION

As at 30 September 2020

| | GROUP | | COMPANY | |
|---|---|---|---|---|
| | 30 Sept 2020 Audited Tzs' 000' | 30-Sept-2019 Audited Tzs' 000' | 30 Sept 2020 Audited Tzs' 000' | 30-Sept-2019 Audited Tzs' 000' |
| **CAPITAL EMPLOYED** | | | | |
| Share capital | 466,431 | 466,431 | 466,432 | 466,432 |
| Share premium | 4,048,462 | 4,048,462 | 4,048,463 | 4,048,463 |
| Properties revaluation reserve | 554,688 | 582,169 | - | - |
| Retained earnings | (17,890,720) | (14,659,031) | (7,835,157) | (6,250,099) |
| **Equity attributable to owners of Co.** | (12,821,139) | (9,561,968) | (3,320,262) | (1,735,204) |
| Non-controlling interests | (2,667,808) | (1,713,323) | | |
| **TOTAL EQUITY** | (15,488,947) | (11,275,291) | (3,320,262) | (1,735,204) |
| **Non-current liabilities** | | | | |
| Borrowings | 1,927,033 | 11,346,457 | 200,006 | 8,647,597 |
| Deferred capital grant | 130,272 | 150,551 | - | - |
| Deferred income tax liability | 85,477 | 139,177 | - | - |
| Retirement benefit obligations | 704,599 | 826,678 | 7,960 | 6,583 |
| Lease liabilities | 926,051 | - | - | - |
| | 3,773,431 | 12,462,862 | 207,966 | 8,654,180 |
| | (11,715,516) | 1,187,571 | (3,112,296) | 6,918,976 |
| **REPRESENTED BY** | | | | |
| **Non-current assets** | | | | |
| Property, plant and equipment | 9,237,971 | 9,763,675 | - | - |
| Right use-of-asset | 958,682 | - | | |
| Investment in subsidiaries | - | - | 5,783,271 | 5,783,271 |
| Loan receivable | - | 279,244 | - | - |
| Deferred income tax asset | - | - | - | - |
| | **10,196,653** | **10,042,919** | **5,783,271** | **5,783,271** |
| **Current Assets** | | | | |
| Inventories | 5,920,666 | 4,427,019 | - | - |
| Trade and other receivables | 4,855,041 | 5,383,758 | 2,331,488 | 1,750,559 |
| Prepaid land rent | - | 20,481 | - | - |
| Cash and cash equivalents | 72,033 | 51,644 | 23,674 | 29,989 |
| Tax recoverable | 441,560 | 466,606 | 375,656 | 374,353 |
| | **11,289,300** | **10,349,508** | **2,730,819** | **2,154,901** |
| **Current liabilities** | | | | |
| Embedded derivatives | 760,265 | 302,618 | 760,265 | 302,618 |
| Borrowings | 27,738,516 | 14,409,204 | 10,148,069 | - |
| Trade and other payables | 4,636,885 | 4,493,033 | 718,052 | 716,578 |
| Lease liabilities | 65,803 | - | - | - |
| | 33,201,469 | 19,204,855 | 11,626,386 | 1,019,196 |
| **Net current liabilities** | (21,912,169) | (8,855,348) | (8,895,567) | 1,135,705 |
| | **(11,715,516)** | **1,187,571** | **(3,112,296)** | **6,918,976** |

### STATEMENT OF CASH FLOWS

For the period ended 30 September 2020

| | GROUP | | COMPANY | |
|---|---|---|---|---|
| | 30 Sept 2020 Audited Tzs' 000' | 30-Sept-2019 Audited Tzs' 000' | 30 Sept 2020 Audited Tzs' 000' | 30-Sept-2019 Audited Tzs' 000' |
| **Cash from Operating Activities** | | | | |
| Profit /(loss) before tax | (4,083,319) | (5,640,390) | (1,585,058) | (715,303) |
| Adjustments for : | | | | |
| Income tax expenses recognised in P & L | | | | |
| Fair value loss on embedded derivatives | 457,647 | 178,907 | 457,647 | 178,907 |
| Depreciation | 700,942 | 648,902 | - | - |
| Depreciation on right os use assets | 89,944 | | | |
| Amortisation of deferred capital grant | - | (20,279) | | |
| Amortisation of prepaid land rent | 20,481 | (13,415) | | |
| Employees Gratuity | (122,079) | (57,953) | 1,377 | - |
| Interest Expenses | 1,553,140 | 1,286,719 | 193,361 | 149,831 |
| Interest on lease liabilities | 90,832 | - | | |
| Interest income | - | - | - | (164,480) |
| Other non cash | - | 813,116 | | |
| Unrealised exchange loss on terms loans | | (105,735) | | 37,324 |
| Other noncash (investment in KTPC W/O) | - | - | | 6,061,763 |
| Profit/ (loss) on disposal of subsidiary | - | 1,944,400 | - | (5,501,827) |
| Changes in working capital: | | | | |
| Inventories | (1,493,647) | 1,448,894 | - | - |
| Receivables | 528,717 | (758,396) | (580,929) | (103,317) |
| Payables | 143,852 | (257,140) | 1,474 | 151,479 |
| Loans Receivables | 279,244 | - | - | - |
| **Cash generated from operating activities** | **(1,834,248)** | **(532,370)** | **(1,512,128)** | **94,377** |
| Interst paid | (904,313) | (1,069,812) | - | (149,831) |
| Income tax paid | (130,133) | (62,077) | (1,303) | (2,077) |
| Interest paid on lease liabilities | (90,832) | - | - | - |
| Net cash generated/(utilised in) from Operating activities | (2,959,526) | (1,664,259) | (1,513,432) | (57,530) |
| **Cash flow from investing activities** | | | | |
| Purchase of property, plant and equipment | (175,239) | (504,136) | - | - |
| Investment in Subsidiaries/ disposal proceeds | - | 228,956 | - | 228,956 |
| Cash paid for right-of-use- assets | (9,256) | - | - | - |
| Loans to third parties | - | 112,384 | - | - |
| Proceeds from sale of property, plant & equipment | - | | | |
| Net cash (utilized in) /generated from investing activities | (184,495) | (162,796) | - | 228,956 |
| **Cash flow from Financing Activities** | | | | |
| Proceeds /(repayment) borrowings | 6,953,541 | 879,396 | 2,365,488 | 256,552 |
| Repayment of borrowings | (5,837,918) | - | (890,528) | (457,884) |
| Effects of exchange rates on loan | - | 83,792 | 32,156 | 46,588 |
| Payment of principal portion of the lease liability | (55,664) | - | - | - |
| Dividends paid | | | | |
| **Net cash flow from Financing Activities** | **1,059,959** | **963,188** | **1,507,116** | **(154,744)** |
| **Net movement in cash and cash equivalents** | **(2,084,062)** | **(863,867)** | **(6,316)** | **16,682** |
| **Cash and cash equivalents at start of period** | **(9,157,280)** | **(8,293,413)** | **29,989** | **13,307** |
| **Cash and cash equivalents at end of period** | **(11,241,342)** | **(9,157,280)** | **23,673** | **29,989** |

### STATEMENT OF CHANGES IN EQUITY

For the period ended 30 September 2020

| Group | Share capital | Share premium | Accum. Losses | Properties revaluation reserve | Othe reserves | Non-controlling interests | Total |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Tzs' 000' | Tzs' 000' | Tzs' 000' | Tzs' 000' | Tzs' 000' | Tzs' 000' | Tzs' 000' |
| **For the period ended** | | | | | | | |
| **30 September 2020** | | | | | | | |
| At start of year | 466,431 | 4,048,462 | (14,659,031) | 595,507 | (13,338) | (1,713,323) | (11,275,291) |
| Transition adjustment | | | | | | | |
| Changes on initial application of IFRS | | | (19,079) | | | (9,778) | (28,857) |
| Profit /(loss) for the period | | | (3,240,092) | | | (944,707) | (4,184,799) |
| Other comprehensive income | | | | | | | - |
| Elimination noncontrolling interest KTPC | | | | | | | - |
| Amortisation of excess depreciation revaluation | | | 39,259 | (39,259) | | | |
| Deferred tax on depreciation transfer | | | (11,778) | 11,778 | | | |
| **As at 30 September 2020** | **466,431** | **4,048,462** | **(17,890,720)** | **568,026** | **(13,338)** | **(2,667,808)** | **(15,488,947)** |
| **For the year ended** | | | | | | | |
| 30 September 2019 | | | | | | | |
| At start of year | 466,431 | 4,048,462 | (11,754,389) | 595,507 | (849,984) | 929,399 | (6,564,574) |
| Comprehensive income | | | | | | | |
| Total comprehensive income for the year | - | - | (2,917,979) | | | (2,776,802) | (5,694,781) |
| Other comprehensive income | | | | | | | |
| Elimination of other reserve on disposal of KTPCL | | | | | 849,984 | | 849,984 |
| Elimination of non controlling interest on disposal of KTPCL | | | | | | 134,080 | 134,080 |
| Amortizations | | | 13,338 | | (13,338) | | - |
| Changegs in ownership of subsidiary | | | | | | | - |
| Final dividend | | | | | | | - |
| **As at 30 Septemer 2019** | **466,431** | **4,048,462** | **(14,659,031)** | **595,507** | **(13,338)** | **(1,713,323)** | **(11,275,291)** |

| Company | Share capital | Share premium | Retained earnings | Total |
|---|---|---|---|---|
| | Tzs' 000' | Tzs' 000' | Tzs' 000' | Tzs' 000' |
| **30 September 2020** | | | | |
| At start of year | 466,431 | 4,048,462 | (6,250,098) | (1,735,205) |
| Comprehensive income | | | (1,585,058) | (1,585,058) |
| Loss for the period | | | | - |
| Actuarial loss net of tax | | | - | - |
| **As at 30 September 2020** | **466,431** | **4,048,462** | **(7,835,156)** | **(3,320,263)** |
| **30 September 2019** | | | | |
| At start of year | 466,431 | 4,048,462 | (32,968) | 4,481,924 |
| Comprehensive income | - | - | | - |
| Profit / (loss) for the year | - | - | (6,217,130) | (6,217,130) |
| **As at 30 September 2019** | **466,431** | **4,048,462** | **(6,250,098)** | **(1,735,206)** |

**Note : The audited accounts were signed by the Auditors on 25 March 2021.**
**The Annual General Meeting of shareholders will be held on 29 April 2020 at 15:00 hours at Protea Hotel, Courtyard, Sea View Ocean Road, Dar es Salaam. Notice will be mailed in due course.**

Vimalendu Kumar Tewari
Company Secretary
**Tatepa Limited**
P.O. Box 700,
Tukuyu, Mbeya.

27 March 2021

Rungwe Avocado Company

WAKULIMA TEA COMPANY LIMITED
TUKUYU-RUNGWE
KATUMBA & MWAKALELI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hatua madhubuti zichukuliwe kukomesha mauaji ya kikatili

**KATIKA** siku za karibuni, kumeripotiwa matukio ya mauaji katika maeneo mbalimbali ikiwamo katika mikoa ya Njombe na Kagera. Mauaji hayo yameibua hisia na mshtuko miongoni mwa Watanzania na hata vyombo vya ulinzi na usalama, hasa polisi, kutoa onyo kali kwa watu wanaoendeleza vitendo hivyo.

Mkoani Njombe. Mke na mume wameuawa kinyama kisha miili yao kutupwa kwenye misitu huku mkoani Kagera, ikiripotiwa wanafunzi wa darasa la nne, akibakwa, kupigwa hadi kufa na baadaye wahusika kumtupa kichakani.

Tukio kubwa la kusikitisha ni lile lililotokea juzi Buhigwe mkoani Kigoma kwa watu wasiojulikana kumuua mwananchi mmoja kwa kumkata kichwa kisha kutoweka nacho kusikojulikana.

Matukio hayo yanaanza kuleta hofu na taharuki miongoni mwa Watanzania ambao kwa muda mrefu wamekuwa katika hali ya amani na usalama.

Awali, matukio kama hayo yalikuwa yakisikika au kushuhudiwa miaka kadhaa iliyopita hasa yale yaliyokuwa yakihusisha mauaji ya watu wenye ualbino na mila potofu. Mauaji hayo ya albino yalizidi kutokana na watu kuwa na dhana potofu kwamba ngozi ya mtu mwenye ualbino inaleta bahati katika biashara au uchimbaji madini pamoja na kupandishwa cheo kazini.

Kadhalika majuaji ya vikongwe yalishamiri kutokana na madai kwamba ni wachawi. Hali hiyo ilihanikizwa kwa kiasi kikubwa na ramli chonganishi hasa katika mikoa ya Kanda ya Ziwa kwa madai kuwa vikongwe hao wanauawa kwa madai kwamba ni wachawi.

Hata hivyo, baada ya vyombo vya dola, asasi zisizo za kiserikali, wanasiasa na mashirika ya kimataifa kupaza sauti, hatua kali zilichukuliwa ikiwamo kukamatwa na kupelekwa mahakamani watuhumiwa ambao baadhi yao walifungwa baada ya kupatikana na hatia.


Hatua hiyo ilipunguza wimbi la mauaji ya vikongwe na watu wenye ulemavu wa ngozi na kuwafanya watu wa makundi hayo kuishi kwa amani huku wakihakikishiwa pia ulinzi kutoka vyombo vya dola.

Lakini sasa suala hili la mauaji ya kinyama lililoibuka sasa, limeamsha jamii kutoka usingizini kwamba vitendo hivyo vimeanza kurudi na kutishia usalama wa wananchi. Ni wakati sasa vyombo vya ulinzi na usalama vikaamka na kutokomeza vitendo hivyo ambavyo si tu ni vya kinyama, bali vinatoa taswira mbovu ya Tanzania katika jumuiya ya kimataifa hususan kwenye ukiukwaji wa haki za binadamu.

Tunatambua kwamba baadhi ya watuhumiwa wa vitendo hivyo wako chini ya ulinzi wa polisi huku upelelezi ukiendelea na watafikishwa kwenye mikono ya sheria wakati wowote.

Pamoja na hayo, ni rai kwamba vyombo vya ulinzi na usalama pamoja na wananchi kwa ujumla kwenye maeneo yao, wachukue tahadhari pamoja na kudhibiti uwezekano wa kutokea vitendo hivyo. Hiyo inawezekana kama kila mmoja atatimiza wajibu wake na kusimama kwenye nafasi yake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Wananchi katu wasiwe pembeni uboreshaji miundombinu ya afya

**AFYA** ni moja ya sekta nyeti katika mustakabali wa maisha ya jamii, mtu anapokuwa afya bora inamuwezesha kufanya shughuli zake kwa ufanisi na kujiletea maendeleo.

Kutokana na umuhimu huo, serikali imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali za kusogeza huduma za afya karibu na wananchi, kwa kujenga zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya na za mikoa.

Hatua hiyo inalenga kuwafanya wananchi kupata huduma za afya mahali popote walipo, iwe ni mijini au vijijini, ikiwa ni tofauti na enzi hizo ambapo huduma za afya zilipatikana kwa wingi maeneo ya mijini.

Ikumbukwe kuwa kabla ya Tanganyika kupata uhuru mwaka 1961, huduma nyingi za afya zilikuwa mijini, lakini sasa zimesogezwa kwa wananchi wa vijijini, ikiwa ni jitihada za serikali za kutaka kila kijiji kuwa na zahanati.

Lakini pamoja na jitihada hizo, zipo baadhi ya kasoro ambazo imebidi Rais Samia Suluhu Hassan aagize mamlaka husika kuzishughulikia ili wananchi wapate huduma za afya bila usumbufu.

Juzi rais alimwagiza Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Ummy Mwalimu kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya sekta ya afya ikamilike kwa wakati.

Katika hotuba yake wakati akiapisha baadhi ya watendaji wa serikali, anaagiza kuendelea kwa ujenzi wa hospitali za wilaya, vituo vya afya na zahanati, lakini pia kuhakikisha vinawekewa dawa na vifaa tiba.

Kauli hiyo inaonyesha kuwa hakuna dawa na vifaa tiba kwenye baadhi ya zahanati na vituo vya afya, hivyo ni wazi kwamba ujenzi unaoendelea hauna budi kwenda sambamba na kuwapo kwa huduma hizo.

Ujenzi wa zahanati kwa kila kijiji, kituo cha afya kwa kila kata na hospitali kwa kila wilaya ni njia ambayo itarahisisha upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi ili waweze kuwa na afya bora.

Hivyo, ni vyema kile ambacho rais ameagiza kikafanyia kazi, hasa upatikanaji wa dawa na vifaa tiba, kwani afya bora ni rasilimali muhimu kwa binadamu na inasaidia kuchangia katika maendeleo yake ya kiuchumi.

Kuwapo kwa dawa na vifaa tiba kutasaidia kutawaondolea kero wananchi kutembea umbali mrefu kufuata huduma ya afya wakati kwenye eneo lao kuna zahanati au kituo cha afya, lakini hakuna dawa.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, anapewa jukumu la kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya sekta ya afya ili wananchi wanufaike na huduma husika.

Pamoja na hayo, ingependeza kama wananchi watashirikishwa katika ujenzi wa zahanati, vituo vya afya na hospitali katika maeneo yao ili kuharakisha ukamilishaji wa huduma hiyo.

Afya ni ni rasilimali muhimu kwa binadamu, hivyo si vibaya wananchi nao wakachangia fedha au nguvukazi, kwa kuwa ndiyo wanufaika wakubwa wa huduma hiyo kwenye maeneo hayo.

Kinachotakiwa ni kuwahamasisha wananchi ili waelewe umuhimu wa kushiriki kwenye shughuli za maendeleo kwenye maeneo yao ili wawe na mchango kwenye ujenzi wa zahanati, vituo vya afya na hospitali.

Serikali imekuwa ikitoa fedha kwa halmashauri mbalimbali nchini, kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya na hospitali za wilaya, lakini pia wananchi kwenye maeneo husika ni vyema wakashiriki katika ujenzi huo.

Yapo baadhi ya maeneo nchini, wananchi wamekuwa wakichangia fedha, wengine kusomba, mawe, maji, mchanga na kokoto ili kufanikisha ujenzi huo na kuharakisha jitihada za kila kijiji, kata na wilaya kuwa na huduma hiyo.

Wakati wananchi wanashirikishwa katika ujenzi huo, jukumu la kuhakikisha kila zahanati, kituo cha afya na hospitali, vyote vinakuwa na vifaa tiba, ni la serikali yenyewe ambayo imeelekeza kuwapo huduma hiyo.

Kutokuwapo kwa dawa na vifaa tiba kwenye baadhi ya zahanati au vituo vya afya, kunawafanya wananchi kukosa ari ya kushiriki katika ujenzi huo, hivyo ni muhimu kutekeleza agizo la Rais.

SAFU

AFYA

# Faida za nyanya chungu mwili wa mwanadamu



Na Nwandishi Wetu

NYANYA chungu ni tunda ambalo wengi wamekuwa wakilitumia katika milo mbalimbali. Tunda hilo hutumika kama mboga au kiungo kimojawapo katika kunogesha mboga.

Katika baadhi ya familia, mathalan, ni mara chache kukuta nyama au samaki, au mboga za majani kama mnafu au majani ya kunde yakiwa hazijapikwa kwa kuchanganywa na nyanya chungu.

Wengine hutumia nyanya chungu, maarufu kama ngogwe, kwa kuchanganya na nyanya na vitunguu ili kupata kachumbari. Vilevile wako baadhi ya watu ambao ama huzitafuna zikiwa mbichi au hupika mboga kwa kuchanganya na bamia au bilinganya.

Kutokana na kuongezeka kwa utaalamu na uzalishaji wa mbegu mbalimbali za mazao, hivi sasa kuna mafungu takriban mawili ya nyanya chungu, fungu la kwanza ni zile nyanya chungu zilizokuwapo tangu zamani ambazo ni chungu na zina rangu ya kijani. Lakini hivi sasa ziko ambazo nyeupe ambazo si chungu. Vijana wa mtaani wanaziita nyanya chungu za mwendokasi.

Pamoja na watu wegi kutumia kama sehemu ya mlo, ni wachache mno wanaojua faida zake kiafya.

Licha ya kufanya mboga kuwa na ladha na harufu ya aina yake, nyanya chungu zina kazi kubwa katika mwili wa binadamu ikiwa ni pamoja na kujenga na kuimarisha afya ya mlaji.

Nyanya chungu ziko katika kundi la jamii ya mboga zenye virutubisho vingi vikiwamo vitamin A, B, na C ambazo zote kwa pamoja hufanya kazi ya kuboresha afya ya mwili kwa ujumla.



**KUSAIDIA MZUNGUKO WA DAMU**

Aidha, ndani ya nyanya chungu kuna Vitamin K inayosaidia kuipa nguvu mishipa ya damu, hivyo kusaidia mzunguko wa damu katika mwili wa binadamu.

Licha ya kuwa karibu asilimia 90 ya nyanya chugu ni maji, mboga hii ina madini ya chuma na potassium hivyo kusaidia uimara wa mifupa.

**KINGA YA MWILI**

Nyanya chungu pia husaidia kuimarisha kinga ya mwilli na kumsaidia mlaji kuepukana na magonjwa ya mara kwa mara.

Mboga hii pia ni kinga inayoweza kumwepusha mlaji kupata maradhi ya moyo au tumbo kujaa gesi au hutoa kinga kwa wanaume wasipate na ugonjwa wa ngiri.

**KIBOKO YA KISUKARI**

Kwa wagonjwa wa kisukari, nyanya chungu ni dawa inayoweza kusaidia katika kupunguza kiwango cha sukari mwilini, hivyo katika chakula chako ni muhimu sana kula nyanya chungu japo kwa wiki mara mbili au tatu.

**KWA WANANDOA**

Hii ni habari njema kwa wanandoa. Nyanya chungu husaidia katika kuongeza nguvu za uzazi kwa wanaume na inatibu pia wale wenye ugonjwa wa ngiri.

Mbali na sifa hiyo, nyanya chungu pia husaidia kuongeza stamina na uwezo wa kuvumilia na kudumu kwenye tendo la ndoa kwa muda mrefu kati ya mume na mke wote endapo watakuwa wanatumia nyanya chungu katika utaratibu unaotakiwa kitaalam (mchemsho).

**MARADHI YA MOYO**

Hizi pia ni kinga iayoweza kumwepusha mlaji kupata maradhi ya moyo. Kutokana na umuhimu huo, mtu anashauriwa kutumia mara kwa mara nyanya chungu ili kumlinda dhidi ya hatari ya kukumbwa na maradhi ya moyo.

**KUUA WADUDU**

Ngogwe ni dawa inayofanana na 'antibiotic', hivyo ni tunda zuri endapo litatumiwa mara kwa mara, husaidia kuua vijidudu vya aina mbalimbali mwilini.

Sambamba na manufaa hayo kwa mwili wa binadamu, nyanya chungu pia zina faida mbalimbali zikiwamo;-

- Kuimarisha kinga ya mwili
- Kurekebisha mzungumko wa hedhi kwa wanawake.
- Kutibu matatizo ya tumbo la uzazi, kusafisha na kulinda mfuko wa uzazi.

MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# ATCL ushindani ndiyo siri ya maendeleo



Na Joseph Kulangwa

**Zikawapo bendi za hapa hapa, za OTTU Jazz au Msondo Ngoma na Mlimani Park maarufu kama Sikinde, nazo zikiwa na ushindani mkali kama ilivyokuwa zamani baina ya Morogoro Jazz na Cuban Marimba za Morogoro.**

TANZANIA kuna timu mbili kubwa shindani za soka na kuna wakati wengine huzita timu hasimu. Nazo ni Simba na Yanga. Hizi hushindana kila sekunde, dakika, saa, siku, wiki, mwezi, mwaka na kila muongo.

Bila ushindani huo, Watanzania mashabiki na wapenzi wa soka wasingekuwa wanapata burudani wanayoipata hivi sasa, wasingekuwa wanafurika viwanjani zinapokutana.

Na bila ushindani huo, moja kati ya hizi mbili kongwe, ingeshafariki dunia na kubaki historia kwamba kulikwa na timu inaitwa Simba au Yanga.

Siku zote na miaka yote, timu hizi zimejitahidi kubaki kwenye ulimwengu wa soka, tena kwa sababu moja ndogo tu, ya nimshinde Yanga au nimshinde Simba, mengine ya fedha na nini ni matokeo.

Watanzania na hata Waafrika Mashariki, hufurahi kusikia Simba imemfunga Yanga au Yanga imemfunga Simba, ndicho huwa kilele cha burudani yao, mengine huwaachia viongozi na wachezaji.

Katika historia ya timu hizi, kuna wakati moja ilikaribia kushuka daraja, lakini kikafanyika kilichofanyika ikanusurika, na lazima kilichofanyika kakilifanyika ili kuhakikisha burudani inaendelea kutokana na ushindani.

Kulipata kutokea pia ushindani wa bendi za muziki wa rhumba za Maquiz du Zaire na Safari Sound, zote za Dar es Salaam lakini zilizosheheni wanamuziki wenye asili ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) enzi hizo ikijulikana kama Zaire.

Zikawapo bendi za hapa hapa, za OTTU Jazz au Msondo Ngoma na Mlimani Park maarufu kama Sikinde, nazo zikiwa na ushindani mkali kama ilivyokuwa zamani baina ya Morogoro Jazz na Cuban Marimba za Morogoro.

Wakati wa ushindani wa makundi haya ya michezo na muziki, soka limeendelea kuwa juu. Hivi sasa Tanzania inasifika kwa soka, tunaona Simba inavyochanja mbuga katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika. Ushindani na Yanga umechangia kufikisha hapo ilipo.

Ni bahati mbaya kwamba bendi za muziki nyingi zimedhoofika kama si kufa, lakini ni kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo za kiuchumi na vifo vya baadhi ya wanamuziki, vinginevyo ushindani ungeendelea zingekuwa mbali.

Nimerudi nyuma kwenye historia, baada ya kumsikia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) katika ripoti yake, akielezea Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) lilivyopata hasara.

Inawezekana kupata hasara kwa shirika hilo, hakushtui lakini kunauma sana hasa jinsi lilivyofufuliwa kwa hainehaine nyingi na ndege kununuliwa mfululizo, lakini leo kubainika ni hasara tupu!

Lipo la kujiuliza na kulitazama upya na kuona wapi lilijikwaa na ndiyo sababu hata Spika wa Bunge, Job Ndugai, akatoa rai kwa wabunge, kujadili na kuona kama kuna haja ya kuendelea kuagiza ndege zingine.

Lakini la harakaharaka bila kuangalia kiufundi zaidi na kitaalamu, kukosekana kwa ushindani kwa kampuni hiyo, ni suala la msingi pia kuangaliwa, kwa sababu bila ushindani kibiashara, lazima kuna kubweteka kuwa "mimi ndiye mimi hakuna mwingine!"

Kulikuwa na shirika la ndege la FastJet ambalo lilionekana kuwa na msuli, ambao bila shaka wenye ATCL yao waliogopa wakidhani misuli ile itaua shirika lao, hivyo kikafanyika kilichofanyika, likatupiliwa mbali virago.

Katika hali ya kushangaza, siku moja Waziri aliyekuwa na dhamana ya kusimamia usafiri wa anga, akainuka mbele ya Rais wa wakati huo na kujigamba: "Mheshimiwa Rais, wamebipu sisi tumewapigia!" Tena kwa bashasha kabisa kana kwamba alikuwa ameua adui, kumbe ameua mshindani ambaye alikuwapo kumwamsha usingizini.

Yanga akiuawa leo, jua hakuna Simba na hali kadhalika Simba akiuawa leo, Yanga haipo. Mbona Coca Cola inakubali kukaa barabarani na Pepsi Cola na watu wanakunywa? Mmoja akiuawa, kuna siku tutanyweshwa chai ya rangi kwenye chupa ya Coca Cola au Pepsi Cola na tuamini ni soda.

**Alamsiki!**

## KONA YA UKWELI

# Misuguano ya viongozi dhidi ya wakurugenzi Mbozi haina tija



Na Thobias Mwanakatwe

SONGWE ni kati ya mikoa 31 ya Tanzania ukiwa umemegwa kutoka Mkoa wa Mbeya mwaka 2016. Jina la mkoa huo limetokana na lile la Mto Songwe ambao unapeleka maji yake katika Ziwa Rukwa.

Mkoa wa Songwe una halmashauri sita ambazo ni Ileje, Mbozi, Songwe, Momba na Halmashauri ya Mji wa Tunduma. Kwa leo nitajikita kuizungumzia Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi ambayo iko mjini Vwawa ambayo ndiyo makao makuu ya mkoa.

Tangu utawala wa serikali ya awamu ya tano uingie madarakani chini ya aliyekuwa Rais, Hayati Dk.John Magufuli, halmashauri hiyo imeongozwa na wakurugenzi wawili ambao ni Kazimbaya Makwega na Hanji Godigodi. Makwega ambaye alileta mageuzi makubwa katika halmashauri hiyo, Mei 2019 uteuzi wake ulitenguliwa na Hayati Dk. Magufuli.

Rais alitangaza uamuzi wa kumtumbua Makwega katika kikao cha kazi kati yake na wakuu wa mikoa, makatibu tawala wa mikoa, wakuu wa wilaya, makatibu tawala wa wilaya na wakurugenzi wa halmashauri.

Ukichimba kwa undani, utabaini chanzo cha Makwega kutumbuliwa ni mgogoro kati yake na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi kipindi hicho na Mkuu wa Mikoa wa Songwe.

Makwega hakupendwa kabisa na viongozi hao hasa baada ya kufanikiwa kudhibiti ulaji wa fedha za ushuru wa kahawa. Alikuta makusanyo yatokanayo na kahawa yalikuwa Sh. bilioni moja na kuyapandisha hadi kufikia Sh. bilioni mbili.

Kutokana na kupanda kwa makusanyo, fedha hizo zilipelekwa kukamilisha ujenzi wa maboma ya shule na zahanati ambayo yalikuwa yametekelezwa kwa muda mrefu bila kukamilika, hivyo kuzua malalamiko mengi kutoka kwa wananchi.

Mgogoro ulipamba moto zaidi pale Makwega alipopambana kupinga kuuzwa kwa gari la halmashauri 'shangingi' kwa thamani ya Sh. milioni nane. Aliyetaka kulinunua alikuwa mwenyekiti wa halmashauri wa kipindi hicho.

Taarifa ambazo sina shaka nazo kabisa, katika migogoro yote hiyo Makwega alichukiwa na baadhi viongozi ambao kwa mtazamo wao walimwona anaharibu ulaji wao.

Makwega baada ya kutumbuliwa kwenye ukurugenzi hivi sasa yuko jijini Dodoma akiendelea na majukumu mengine.

Baada ya Makwega kutumbuliwa, bahati ikamwangukia mwanamama shupavu, Hanji Godigodi. Mwanamama huyu ni mzoefu katika kazi ya ukurugenzi kwa kuwa kabla ya kupelekwa Mbozi, ameshawahi kuwa mkurugenzi katika halmashauri kadhaa zikiwamo Mbinga na Kigoma ambako historia yake imetukuka na haina doa.

Katika kile ambacho unaweza kusema labda kuna jinamizi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, ikiwa ni miaka miwili tu tangu Makwega atumbuliwe kutokana na sababu nilizozitaja huko juu, mwanamama huyo naye ameanza kuandamwa na viongozi wa chama na serikali wa mkoa huo.

Sababu za kuandamwa kwake hazitofautiani na zile zilizosababisha Makwega kutumbuliwa ambazo ni kusimama kidete kupinga ubadhilifu wa fedha za halmashauri unaotaka kufanywa na baadhi ya viongozi kama ni jambo lililozoeleka katika halmashauri hiyo.

Taarifa za uhakika ni kwamba mkurugenzi huyo alitishiwa maisha na mmoja wa viongozi wa ngazi za juu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Songwe tena mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Songwe na Katibu Tawala Mkoa huo.

Kisa cha kutishiwa maisha ni baada ya mkurugenzi huyo kukataa kuidhinisha malipo ya zaidi ya Sh. milioni 12 alizotakiwa kulipwa Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa ambazo alidai zimetokana na kuiuzia nondo na saruji halmashauri hiyo.

Mkurugenzi alikataa kuidhinisha fedha hizo kwa hoja, kwanza, akitaka apewe nyaraka za ununuzi wa vifaa hivyo na vilitumika katika ujenzi wa nini kwenye halmashauri hiyo kwa sababu hakukuwa na nyaraka zinazoeleza mambo yote hayo.

Kitendo cha mkurugenzi kukataa kuidhinisha malipo hayo hadi ajilidhishe ndio kimesababisha atishiwe maisha na kibaya zaidi wapo baadhi ya viongozi wa serikali ambao wameungana na mwenyekiti wa chama kumpinga katokana na msimamo wake huo.

Suala hili la kutishiwa mkurugenzi Machi 2, mwaka huu, alitoa taarifa katika kituo kikuu cha polisi Vwawa na kupewa RB ambayo kwa leo sitaiweka wazi kwa sababu maalum.

Sina maslahi yoyote na mkurugenzi huyo lakini ninachojiuliza na sipati jibu, kwa nini kila mkurugenzi anayepelekwa katika halmashauri hiyo lazima ajengewe mizengwe, fitina na umbeya ili mradi tu mamlaka zake za uteuzi zimwondoe.

Nadhani hapa vyombo vinavyochunguza katika suala hili viangalie kwa undani aina ya viongozi wa serikali na chama waliopo katika mkoa huu kwasababu haiwezekani kila mkurugenzi anayepelekwa Mbozi aonekane hafai na kujengewa fitina, hapo kuna tatizo.

Ufike wakati kila kiongozi katika mkoa huo atekeleze wajibu wake kama alivyoapa kwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa nina imani hakuna aliyeapa kufanya ufisadi.

Rais aliyepita, Hayati Dk. Magufuli na hata wa sasa, Samia Suluhu Hassani, wanapinga kwa nguvu zote masuala ya ubadhilifu wa fedha za umma ambao unaonekana kuota mizizi zaidi katika halmashauri.

Ni matumaini yangu kuwa vyombo vyenye dhamana ikiwamo Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) vitatenda haki katika kuchunguza suala hilo ili anayestahili kupewa adhabu apewe kwa mujibu wa sheria za nchi.

**MBOZI BILA UFISADI INAWEZEKANA, MUNGU IBARIKI TANZANIA**

**Kwa maoni na ushauri tuma katika barua pepe mwanakatwe2015@gmail.com au katika WhatsApp 0762-183666.**

## DARASA LA NDOA

# Mambo ya kuzingatia wakati wa uchumba- 2



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka

UCHUMBA huanza na urafiki na mtu anaweza kuwa na marafiki wengi, lakini mchumba huwa ni mmoja tu, ambaye hutokana na marafiki mtu alio nao. Hata hivyo katika kutafuta mchumba yako mambo kadhaa ya kuzingatia na si kukurupuka tu kwani kufanya hivyo kunaweza kusababisha madhara makubwa katika maisha.

Katika sehemu ya kwanza ya makala hii, tulijadili baadhi ya mambo ya sehemu hii inaendelea kudadavua mambo mengine kwa kina. Kwa mantiki hiyo, pamoja na mambo mengine, mtu kabla ya kuingia katika ndoa, anapokuwa kwenye uchumba azingatie yafuatayo kama yanavyobainishwa katika mwendelezo wa mada hii;-

**PIMA UWEZO WAKE**

Maisha ni kusaidiana na kushauriana. Haifai kuwa tegemezi kwa kila kitu hata kwa mawazo. Pima uwezo wa mchumba wako katika kufikiri, kushauri na kufanya uamuzi.

**EPUKA UCHUMBA WA SIRI**

Ndoa si jambo la siri. Unapotaka kuoa huna budi kuwashirikisha wazazi au walezi wako mapema. Kuchagua mwenzi ni wajibu binafsi, lakini ni vyema kushirikisha wazazi au walezi kwa ushauri zaidi.

Vijana wengi siku hizi hawashirikishi wazazi au walezi wao mchakato wa kumpata mwenzi, bali hushirikisha uamuzi ambao wamekwishafanya tayari. Hali hii imesababisha wazazi au walezi wengi kuwa waathirika wa uamuzi utokanao na watoto wao pale matatizo yanapojitokeza.

**MUDA WA KUKUTANA**

Kuzungumza ana kwa ana kunasaidia kufahamiana vizuri zaidi. Ni wakati wa kushirikishana hisia na hali kila mmoja alizonazo. Ni wakati wa kuandaa mpango mkakati wa ndoa.

Wakati wa uchumba ni wakati wa kuwekana wazi kuhusu matarajio katika ndoa. Ni muhimu kila mmoja kuwa muwazi, kwani gharama ya kuficha uhalisia wako ni kubwa baada ya ndoa.

Imani na upendo hufa hivyo uwezekano wa kuvunjika kwa ndoa ni mkubwa, hasa pale mwenzako anapogundua kuwa ulimficha kuhusu jambo fulani wakati wa uchumba.

**PIMENI AFYA**

Suala la afya ni la muhimu katika maisha na ustawi wa ndoa. Kwa sasa tunaishi katika jamii ambayo yako maradhi mbalimbali ya kurithi au kuambukizwa.

Kwa mantiki hiyo, ni muhimu kujiridhisha kuhusu ukamilifu wa afya ya mwili na akili. Hii itasaidia kama kuna matatizo yafahamike na kushughulikiwa mapema, kwani kinga ni bora kuliko tiba.

**KUJIFUNZA KUHUSU NDOA**

Watu wengi huelekeza nguvu zao nyingi katika kuandaa sherehe za harusi huku wakisahau kujiandaa kuwa waume au wake bora. Matokeo yake sisi ni mashahidi wa ndoa nyingi zisizodumu. Ni muhimu kuzingatia kuwa, nyumba hujengwa kwa hekima, ufahamu na maarifa.

Kutokana na ukweli huo, bidii ya kujifunza mambo yanayohusu taasisi ya ndoa ni muhimu sana ili kupata ufahamu na maarifa ya kutosha kuhusu ndoa. Wachumba wafahamu mahitaji na madai ya taasisi ya ndoa kabla ya kufanya uamuzi wa kuingia katika ndoa.

Wachumba pia wawe na kiu ya kufahamu misingi, kanuni, na taratibu za ndoa mapema, kwani wakishakuoana maisha hayatakuwa kama walivyozoea. Mfumo wa maisha unabadilika. Hivyo, wajiandaye kuyakabili mabadiliko na maisha mapya.

**TOFAUTI YA UMRI**

Wasichana hupevuka haraka zaidi kuliko wavulana kwa sababu za kibaiolojia na kimaumbile. Hali hiyo husababisha wasichana kukua haraka, kuwa na fikra na mitazamo ya juu zaidi kuliko wavulana (IQ).

Pamoja na kwamba umri unaweza usiwe kigezo kwa wapendanao, inashauriwa kuwa, umri wa mwanaume anayekusudia kuoa awe miaka mitano (5) na zaidi na asizidi miaka kumi (10) ya umri wa mwanamke ili waweze kuendana.

Kinyume na hapo, kadri miaka inavyokwenda na majukumu ya kifamilia yanavyoongezeka, yuko atakayeonekana ni kijana sana na mwingine ataonekana ni mzee (kachoka). Matokeo yake ni mtu kutojiamini, kukosa ujasiri, kukwepana na kutokupenda kuambatana pamoja.

**UTAJUAJE NDIYE?**

Hili ni swali la msingi ambalo vijana wengi hujiuliza wanapokuwa katika hatua ya uchumba. Yafuatayo ni mambo ya kukusaidia ili kujibu kiu ya swali lako.

Yule ambaye ndiye, utamjua kwa kuangalia mambo yafuatayo:

- Anachukua sehemu kubwa ya moyo na mawazo yako.
- Unajisikia amani na furaha moyoni.
- Ngono, mali, fedha au vitu si kipaumbele chake. Anakupenda jinsi ulivyo.
- Anatamani sana uwapo wako.
- Anapenda mawasiliano ya mara kwa mara.
- Anaonyesha moyo wa kujali na kuthamini.
- Anaonyesha hali ya kuwa mvumilivu na subira.
- Si king'ang'anizi wala mtu wa haraka na papara.
- Anaonyesha uwezo wa kuchukuliana na hali yako.
- Anakuheshimu na kujiheshimu.
- Anakubalika na wazazi au walezi wako.

**Itaendelea Jumapili ijayo**

**Dk. Mlyuka ni mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maoni, mafunzo na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255 744000066.**

# MAISHA

APRILI 11, 2021
Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*



Ukurasa 10

## Anatembea kike, nani wa kulaumiwa?



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Fanya haya kupendezesha mandhari ya nyumba yako



## HARUSI

Ukurasa 12



## USIJIKONDESHE

# Hipsi hujengwa kwa mazoezi

Ukurasa 14

# Anatembea kike, nani wa kulaumiwa?

Na Moses Ismail

"NAJISIKIA tumbo la uzazi linauma kila ninapomwangalia huyo kijana mwonekano wake wa siku hizi, jinsi anavyovaa, anavyotembea yaani naumia," anatamka mama nisiyemfahamu ambaye nilikuwa naye karibu kwenye kituo cha daladala eneo la Boma, jijini Dar es Salaam.

Kauli yake inanigutusha, nami nalazimika kuangalia kule anakoangalia yeye.

"Kwani wewe unamfahamu vizuri huyu kijana, nimewahi kuonana naye na kila anapokatiza ndiyo hivyo watu wengi wanamshangaa," mwanamke mwingine wa upande wa pili wa yule mama anajibu.



Wakati huo macho yangu yanamfuatilia kijana anayezungumzia, binafsi ni kweli mwonekano wake unasababisha maswali kadhaa, ni kijana wa kiume lakini mwendo wake una madoido ya kike na amejipodoa kwa namna fulani hivi.

Anazusha mjadala usio rasmi kwa baadhi ya abiria waliokuwa pale kituoni, wapo wanaolaumu wazazi wake kuwa walishindwa kumlea vizuri na kumpa uhuru uliomfanya awe vile alivyo.

Ukweli ni kwamba jukumu la malezi limegawanyika kuna mahali linawahusu wazazi, upande mwingine waalimu na kwingine ni jamii inayomzunguka.

Ushirikiano unahitajika katika kumlinda mtoto kwenye makuzi yake kwa kuwa mzazi kuna wakati anakuwa kwenye kusaka kipato mtoto anakwenda shule au anashinda nyumbani kama hajafikisha umri wa kwenda shule. Mzazi anapaswa kutambua mazingira ambayo mtoto wake anakuwa kama ni shuleni au ni nyumbani je, kuna usalama wa namna gani?

Ni wazi kuwa wazazi wanaweza kujisahau hasa watoto wanapokwenda shuleni, wengine hawawapi huduma zinazostahili pengine kwa kutokuwa na uwezo na wengine kutoona umuhimu ndipo walimu wanapobaini udhaifu huo na mwingine huwashtua wazazi.

Mfumo wa malezi kwa watoto umekuwa na shida kwa namna moja kutokana na mila na tamaduni kutofautiana kulingana na kabila la mzazi.

Kuna baadhi ya tamaduni na mila ambazo huthamini ulinzi wa watoto wa kike wakiamini kwamba ndiyo wanaopaswa kulindwa kwa kuwa wao ni dhaifu tofauti na wakiume ambao uaminika kuwa ni majasiri hivyo wanaweza kujilinda.

Hapo ndipo makosa yanapoanzia kwa kuwa watoto kadhaa wa kiume wamekuwa huru kwa kuwa wanaaminika, baadhi yao wamejikuta wakijiunga kwenye makundi ya vijana walioshindikana ambao huwafunza mambo maovu.

Miongoni mwa mambo hayo ni pamoja na matumizi ya vileo, ikiwamo uvutaji wa bangi na dawa za kulevya na kwenda kwenye maeneo ya anasa.

Ukweli ni kwamba watoto wanapaswa kupewa ulinzi sawa awe wa kike au wa kiume ni haki yake kulindwa ili aweze kukua katika hatua nzuri zinazostaili.

Ni vyema jamii ikabadilika na kujenga ushirikiano mzuri wa malezi kwa watoto wote, vinginevyo ni kuruhusu kuendelea kuharibika kwa mmomonyoko wa maadili yetu.

Watoto wanapaswa kufundishwa kujitambua na kutunza maumbile yao kwa ujumla, ikiwamo kutoruhusu kushikwa shikwa kwenye nyeti zao, ukaribu na watu ambao hawaeleweki nyendo zao.

Kuendelea kushangaa walioharibiwa na kusikitika haisaidii kitu jamii inapaswa kushirikiana ukatili kwa watoto wote unafanywa kwenye maeneo ambayo wapo wanaoona lakini wananyamaza kimya kwa kuwa siyo watoto wao tu.

Hiyo siyo sawa tambua kama unakwenda hospitali unatibiwa daktari ambaye hata humjui, hata huyo mtoto ambaye unapuuza kusaidia kudhibiti asiharibiwe unazimisha ndoto zake kwani akifanikiwa kutulia na kusoma anaweza kushika nafasi kubwa ya uongozi akasaidia kuiletea jamii na taifa maendeleo.

## QUIZ

NA HAMIS KIDAGO 0657 207168

**Weka maneno yafuatayo katika mtitiriko utakaoyafanya yalete maana kamili.**

**Mfano:** marguerite/est/La/fleur/une - La marguerite estune fleur.

oiseau/Le/un/est/perroquet
……………………………………………………

plantesfragiles/Les/rosiers/des/sont
……………………………………………………

un/saumon/poisson//est/Le
……………………………………………………

est/erable/arbre/un/L'
……………………………………………………

citron/est/Le/fruit/un
……………………………………………………

poireau/un/est/Le/legume
……………………………………………………

des/Le chien et le chat/animauxdomestiques/sont
……………………………………………………

bambou/une/Le/est/herbe
……………………………………………………

qui/méne au success/est/Le/un/pont/fragile
……………………………………………………

c'est/l'histoire/qui commence/Entre/au depart/nous
……………………………………………………

d'avoir/Sois/raison/et puis/sûr/vas-y
……………………………………………………

la durée/le soleil/de la nuit/apparaîtra/Quelquesoit
……………………………………………………

Jibu kama kwenye huo mfano hapo chini.
Mfano: **Tu as une valise?** – Oui, j'aiune valise de mon frère.

Vousavez des chaussures de marche? – Oui, j'ai…….chaussures de monpère.

Tu as un appareil photo? – Oui, j'ai………..appareil photo de moncopain.

Vousavezunetente de camping? – Oui, j'ai…………tente de mon cousin.

Tu as unevoiture? Oui, j'ai……..voiture de mes parents.

Tu as des skis? – Oui, j'ai…….skis de ma sœur.

Vousavezun sac à dos? Oui, j'ai…….. sac à dos de ma tante.

Tu as unstylo? Oui, j'ai………stylo de monvoisin.


Vousavezuneboisson à consommer? Oui, j'ai…….boisson de ma petite amie.

Tu as des lunettes? Oui, j'ai………lunettes de monami.

**Les articles partitifs**
Angalia kwa makini mfano huu wa "articles partitifs" katika maelezo yafuatayo, kisha ujibu maswali yatakayofuata kuhusu hizo "articles partitifs".
**N.B.** (ms) nimasculinsingulier, (fs) nifé mini singulier.
. Cestgentil à toi de faire les courses: alors, s'ilteplaît, tuachetesdu riz (ms), del'eau (fs), de laviande (fs) et de l'huile (fs) et tuprendsde l'argent (ms) dansmon sac.

## WATOTO

# PAKA RANGI







Alichokifanya daktari

HAKUNA watu wenye ndugu wengi kama makonda wa daladala. Ebu msikie konda huyo wa Posta kwenda Makumbusho.

"Haya dada hapo mbele, mjomba kule mwisho kaa vizuri…oyaa mamdogo unaenda? Bibi shuka taratibu, shemeji umeikuta haya panda. Babu njoo ukae! Baba angu hapo tusogee kidogo,"

"Shangazi maliza ngazi,Swaiba geukia mbele, Kaka hapo shika upande wa pili,mdogo wangu mpishe mama mkwe akae," Wakimaliza kazi wana ndugu kibao walioonana nao siku moja tu.

**SWALI**
Mawe ya Matambawe yanapatikana sehemu gani?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Mwenye nguvu atamshinda aliye dhaifu

KARIBU tena msomaji katika safu yetu hii ya Maisha Ndivyo Yalivyo.Wiki iliyopita nilitoa mfano wa kijana ambaye hatua zake za maisha zimefungwa.

Kila mradi anaowekeza anaishia kufilisika na kubaki na madeni na hivyo kukosana na wabia wake wakiwamo nduguze. Jiulize, ni kwa nini mtu anakumbwa na hali kama hiyo?

Ili uwe mshindi ni lazima ushindane. Huwezi kusema unataka ushindi wakati huna nguvu ya kushindana. Siku zote ukiwa dhaifu utashindwa na mwenye nguvu.

Yako aina ya matatizo ambayo lazima uwe na kiwango fulani cha nguvu kuyatatua. Kwa mfano, kila aina ya mateso uliyo nayo, yanahitaji aina ya maombi kwa Mungu ili uweze kuondokana nayo.

Lazima ujue una aina gani ya kifungo kwani kila tatizo lina jinsi yake ya kulitatua. Kuna mzizi wa mti wa mwembe na mizizi ya mpapai. Yote ni mizizi lakini mmoja ni mgumu kuung'oa na mwingine ni mwepesi.

Kila tatizo linalompata mtu lina chanzo chake, lina aina yake. Mtu anapojiona yupo pale pale, hapigi hatua ya mafanikio ni kwa sababu hana nguvu ya kumtoa hapo. Ili uwe na hatua mpya unahitaji nguvu. Siku zote mwenye nguvu ndiye anayeshinda, anayetawala. Hiyo ni kanuni.

Pamoja na ukweli huo, wapo watu wanatakiwa washinde lakini wanazidiwa nguvu na wenzao, wanawarudisha nyuma kama kijana niliyomzungumzia hapo awali. Katika hili, Mungu ameonyesha katika baadhi ya maandiko yako.

Kwa mfano zaburi 88:8, neno linasema "Wanijuao umewatenga nami; umenifanya kuwa chukizo kwao; Nimefungwa wala siwezi kutoka". Adui siku zote hapendi watu wenye nguvu kwani wataendelea kushinda.

Ni ukweli ulio dhahiri kuwa nguvu kubwa inapokutana na nguvu ndogo, ile ndogo inasalimu amri. Wapo watu wanaosubiri nguvu zako zipungue ili wakutese. Wengine wanakusubiri ufikie hatua fulani ya mafanikio, ndipo wanaongeza nguvu ya kukuangusha.

Msomaji wangu, kijana yule niliyemjadili wiki iliyopita, alisema pamoja na mambo mengine kwamba anapata wawekezaji katika miradi mbalimbali lakini hafiki mbali. Matokeo yake miradi inafia mikononi mwake na kuambulia kashfa. Inawezekana mtu wa aina hii aliwahi kujihusisha na ushirikiana ili kufanikiwa. Lakini katika mazingira hayo 'wataalamu' aliowaendea wakamzidi nguvu wakapora nyota yake ya utajiri.

Au kwenye ukoo wake yaliwahi kufanyika maagano, matamko ya kutofanikiwa. Au mmoja wa wanafamilia aliwahi kumtamkia kwamba hatafanikiwa. Maneno ni nguvu, yanaumba. Na shetani ana tabia ya kukuza jambo, hivyo usidharau maneno.

Vile vile ipo mbinu nyingine ambayo maadui huitumia kuharibu hatma ya wenzao. Wakiona wewe unategemewa na familia yako, hufanya jitihada kubwa kukuangusha. Lazima wakutafute kwa nguvu zote.

Hata maandiko ya Mungu yanaonyesha kuwa wale wanaotegemewa hupata misukosuko. Maombolezo 4:20 neno linasema, "walimnasa yule ambaye maisha yetu yalimtegemea..."

Kuna watu leo ni msaada wako, ni chemchem ya mafanikio yako lakini wamepigwa. Shetani huangalia ni nani chanzo cha mafanikio, ushindi au utajiri wako, huyo ndiye anayetafutwa ili asiendelee kukusaidia. Maisha Ndivyo Yalivyo.

Tuwaombee sana viongozi wetu. Wengi wanapigwa na maadui kwa kuwa hawana nguvu ya kulinda vyanzo vya mafanikio yao. Kama wewe ni chanzo cha mafanikio ya familia yako, ni muhimu uwe makini.

Kupitia wewe watoto watasoma, wazazi wataishi vizuri. Kupitia biashara zako ndugu zako watafurahi. Tafuta nguvu ya Mungu kutoka hapo ulipo kwani shetani lengo lake ni kukutoa kwenye kusudi la Mungu ili akutawale. Tuliumbwa tuwe matajiri siyo masikini.

Lakini pia ni vema tukajua kwamba chochote kinachotokea kimesababishwa. Hakuna umasikini usio na chanzo. Kuna kitu lazima ufanye ili kitu kizuri kitokee. Ukitaka kutumiwa na Mungu, nawe utumike sana kuzifanya kazi zake. Wapo wanaopigwa kwa kumsahau Mungu. Wanategemea nguvu za giza badala ya nguvu kubwa ya Mungu.

***Msomaji wangu, naishia hapa hadi wiki ijayo. Naamini umejifunza kitu hapo. Je, una maoni, kisa cha kimaisha? Tuma ujumbe mfupi kupitia 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Nawasalimu kwa jina la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania

NAWASALIMU kwa jina la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania! Itikieni kazi inaendelea. Hii ndiyo salamu ya utambulisho ya Rais wetu wa sita katika serikali ya awamu ya tano, Samia Suluhu Hassan, ambayo ndani yake imebeba umoja, mshikamano, upendo na utaifa kwamba Tanzania ni moja na watu wake ni wamoja.

Yote hayo ndiyo yataimarisha na kuendelea kulijenga taifa la Tanzania, ikiwamo kulitambulisha vyema duniani katika kuendeleza ushirikiano kwa kuwa si kisiwa.

Aidha, hotuba yenye tumaini na nuru mpya kwa Watanzania imeijaza mioyo ya wengi hasa pale Rais aliposisitiza haki itamalaki na kuondoa dhuluma ambayo kwa kiasi fulani ilichangia kuwapo kwa malalamiko makubwa na kuijaza mioyo ya wengi.

Ubabe ulitamalaki baadhi ya maeneo kama kwenye kukusanya kodi kiasi cha misuli kufanya kazi zaidi kuliko akili kiasi cha kukwangua kila kitu na kuua biashara bila kuangalia baadaye itatoka wapi kodi nyingine au watarudi kukusanya wapi.

Sasa ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) iko hadharani na imeibua mengi ambayo yanahitaji usimamizi thabiti katika kuziba mianya ya upotevu wa mabilioni ambayo yangetumika kutoa huduma bora kwa Watanzania.

CAG ametufumbua macho na kuonyesha hasara iliko, udhaifu na amependekeza nini cha kufanya, kwa kuwa fedha zilizopotea zingetumika kuboresha upatikanaji wa dawa hospitalini, maji umbali usiozidi mita 400, miundombinu ya elimu na barabara, lakini sasa tunaelezwa wachache walizichukua.

Ripoti hizi husomwa kila mwaka na huibua mengi ambayo huhuzunisha Watanzania kwamba waliopewa dhamana ya mali ya umma, baadhi wameitumia ndivyo sivyo na kutozingatia taratibu za matumizi ya fedha ya umma.

Swali la kujiuliza ni kwa kiasi gani mapendekezo ya CAG yanafanyiwa kazi? Ni kwa kiasi gani mianya ya upotevu inadhibitiwa? Yote haya Rais Samia aliyagusia katika hotuba yake akitaka uwajibikaji kwa watumishi wa umma ili kufikia malengo tarajiwa.

Iwapo kutakuwa na uwajibikaji, kuishi kwa viapo na kuenenda ipasavyo kwa aliyeajiriwa kutambua, kutunza na kuheshimu dhamana hiyo, maana yake ripoti za CAG hazitatueleza kuwa kuna zaidi ya Sh. bilioni tatu zilitolewa benki na kupelekwa kusikojulikana.

Hatutaambiwa kuwa makusanyo ya Sh. bilioni mbili hayajulikani yalipo au fedha zilikusanywa na hazikupelekwa benki au mkandarasi alilipwa lakini hakufanya kazi.

Mabilioni ya shilingi yanayotajwa ndiyo hayo yangegharamia bima za afya za Watanzania kwa mamilioni ambao leo hii wana bima ndogo na wengine hawana kabisa kiasi kwamba wakipata maradhi makubwa kama ya figo, basi hawawezi kumudu gharama za kubadilisha au kusafisha kila wiki.

Katika hospitali za umma baadhi ya dawa hazipatikani na ni kawaida kabisa unaandikiwa dawa ipo kwenye bima lakini unatakiwa kwenda kununua huku vifaa tiba muhimu navyo hakuna halafu Mtanzania anasikia kuna fedha imechotwa mahali.

Fedha iliyochotwa ni mali ya Watanzania ambayo inatokana na kodi mbalimbali ikiwamo kodi ya ongezeko la thamani (VAT) ambayo inalipwa na Mtanzania wa kawaida kabisa katika kila bidhaa anayonunua. Lakini badala irudi kumsaidia, inakwenda kwenye mifuko ya wachache.

Serikali ya Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dk.John Magufuli, iliweka kipaumbele katika ujenzi wa miundombinu mingi hasa ya barabara zikiwamo za mitaa na sasa mitaa mingi ya Dar es Salaam inapitika vizuri na imesaidia kupunguza foleni.

Licha ya kazi hiyo nzuri, bado sehemu nyingi miundombinu ya mitaa si ya kuridhisha na haipitiki hasa nyakati za mvua na hii ni Dar es Salaam ambayo ni jiji la kiuchumi. Bado kuna miji mingine ambayo inahitaji miundombinu thabiti ili kuharakisha maendeleo.

Uwapo wa miundombinu mizuri utasaidia kupunguza wimbi la kila kijana kukimbilia mjini kuwa mfanyabiashara mdogo, ambao sasa wametapakaa hadi Posta na hawachagui wapi pa kufanyabiashara na pa kuacha.

Iwapo kutakuwa na miundombinu mizuri maana yake hata mzunguko wa fedha utaboreka na nguvu ya watu kununua itaimarika na wengi watapenda kubaki waliko au kwenye miji yao badala ya wote kukimbilia Dar es Salaam.

Wafanyabiashara wadogo si walipakodi bali ni wengi wenye kujitafutia mkate wa siku na kodi itapatikana katika ununuzi wa bidhaa, lakini kusambaa kwao kila mahali kwanza ni kuharibu mandhari ya jiji au mji na kuua biashara za wenye maduka wanaolipa kodi

Mathalani, ukienda Kariakoo kila nje ya duka kuna wafanyabiashara wadogo kiasi kwamba mwenye duka naye anaamua kufunga duka na kuwa na vijana wakuuza biashara zake kwenye vizimba vya muda mfupi.

Nawaza kwa sauti inayaona haya yote kama changamoto kubwa na ili kazi iendelee ni lazima lifanyike jambo kubwa sana. Kwanza, wote waliotajwa kwenye ripoti ya CAG wachukuliwe hatua kama ilivyopendekezwa na waturudishie fedha zetu.

Pili, lazima kuwe na jitihada za dhati kabisa kunusuru biashara za wanaolipa kodi rasmi kwamba wafanyabiashara wadogo wasiruhusiwe kuwapo kila mahali kila wakati kwa sababu tunatengeneza taifa la machinga na kusahau kubwa kodi inahitajika sana katika uendeshaji wa serikali.

Tatu, lazima wateule wawajibike kumsaidia rais kuhakikisha hakuna mkwamo, kuhakikisha taifa linasonga mbele na kupiga hatua kubwa kimaendeleo, vinginevyo tutarudi katika nchi ya uchumi wa chini kutoka kwenye uchumi kwa kipato cha kati cha chini.

***Mungu ibariki Tanzania***

# HARUSI



Chereko na nderemo vilitawala wakati Maimuna Said akifunga pingu za maisha na Abdullah Ismail, katika Msikiti wa Ibadhi ulioko Temeke jijini Dar es Salam juzi.

MITINDO

KIAFRIKA ZAIDI

# Ukivaa hivi hautajutia siku yako



BARA la Afrika limejaaliwa kuwa na tamaduni mbalimbali zinazovutia. Moja ya tamaduni hiyo ni aina ya mavazi yake ambayo yanawatenganisha Waafrika na watu kutoka sehemu nyingine duniani.

Katika suala la mavazi, kumekuwa na aina tofauti ya vitambaa na mwonekano wa ushonaji kulingana na eneo,

Tofauzi zote za mavazi na aina ya ushonaji ni kuleta ladha ya kipeee kwa watu wanaovaa.

Pengine kunaweza kuwa na aina nyingi ya mavazi asilia katika nchi za bara la Afrika, lakini kwa nguo za aina hizi zimekuwa pendwa na mvuto wa kipekee.

**KITENGE**

Hili ni aina ya vazi ambalo asili yake ni Afrika, inatokana na malighafi ya pamba inayopatikana katika nchi zetu.

Vazi la kitenge kwa miaka kadhaa tangu lianze kutumika limekuwa likijipatia ubora na nafasi ya kipekee katika kukua na kuendelea.Wanaume kwa wanawake wamekuwa wakishona mavazi yanayolingana na kuwafanya wavutie.

**BAZEE**

Vazi hili pia halina tofauti sana na kitenge katika sifa na ubora wake Kwani takribani asili ya mavazi yote ya Kiafrika yapo kwa ajili ya kupendezesha na kuboresha mwonekano halisi wa mwafrika.

Vitambaa vya bazee vimekuwa vikipatikana kwa namna tofauti kuanzia ukubwa, rangi na maua yake.Yote hiyo ni kufanya kuwa na mwonekano wa kipekee.

Mpaka sasa hivi tumekuwa tukishuhudia idadi ya watu wengi wakipendelea kushona na kuvaa vazi hili la bazee katika sehemu tofauti kwenye mikutano,sherehe, harusi na ofisini.

**BATIKI**

katika vazi hili uzuri wake huanza kuonekana pale baada ya kutengenezwa kwa jinsi uchanganyaji rangi unavyopendeza machoni.

Vazi hili pia humruhusu mtu yoyote yule kukidhi mahitaji yake katika mitindo ya kushona ambayo inawatoa vilivyo.







URAEMBO



USIJIKONDESHE

# Hipsi hujengwa kwa mazoezi

UREMBO wa mwanamke sio sura pekee, bali siku hizi kuwa na umbo lenye mapaja yaliyoshiba maarufu kama 'Hipsi' ni sifa moja inayozingatiwa kuwa na mwonekano mzuri.

Hipsi kwa mwanamke ni jambo la kujivunia hata kama hana makalio makubwa, kwani umbo hilo linatosha kuwa na mwonekano unaovutia zaidi.

Mtu akiwa na hipsi pana, inamfanya kuwa na umbo la nyigu, yaani kiuno kinakuwa cha wastani na tumbo jembamba kiasi ambacho akilala unaweza kuona alama za mifupa inayokamata mbavu na viungo vingine vya mwili.

Wengine hutumia madawa na baadhi hufanyiwa upasuaji wa kurekebisha nyama.

Njia zote hizo ni ngumu na zinazotumia pesa nyingi kukamilisha hitaji lako, lakini kuna mbinu nyepesi na hazina gharama katika kukamilisha ndoto yako.

Kupitia mazoezi ya kuongeza hipsi unaweza kutengeneza umbo na kuwa na muonekano wa kuvutia.

### MAZOEZI YA SQUAT

Ili kuanza mazoezi haya, simama wima kwa miguu yote kisha fanya kwamba unaketi hewani. Unapofika urefu kama wa mtu aliyeketi kwenye kiti, inuka tena na kusimama wima.

Aina hii ya mazoezi huivuta misuli ya mapaja na kuibana, hivyo basi kuongeza upana wake. Siku za kwanza za mazoezi, utahisi maumivu, lakini baada ya siku kadhaa, utazoea na uchungu kupotea kabisa. Fanya mazoezi haya kwa roundi tatu kila siku.

### MAZOEZI YA BRIDGE

Ili kufanya zoezi hili, lala chini chali, yaani kwa mgongo. Lainisha miguu kabisa na kuiweka mikono karibu na mwili. Kisha uinue kiuno chako juu mpaka uhisi kuwa umefika mwisho.

Bakia kwenye hali hii kwa muda wa sekunde kumi kisha uuinue mguu wa kulia juu. Ukihisi kuwa mguu umefika mwisho, uteremshe mguu wa kulia na uuinue wa kushoto. Rudia zoezi hili kwa mara kumi kwa kila mguu.

Ulifanye zoezi hili kwa raundi tatu kila siku. Unaweza kuongeza idadi hii kulingana na mapenzi yako.

### MAZOEZI YA 'DONKEY KICK'

Zoezi hili linahitaji kuirusha miguu kwa nyuma. Ili kulifanya hivyo, kaa kama mnyama kasha usimame kwa magoti na mikono kama mnyama.

Baada ya hapo, uinue mguu wa kulia kwa nyuma na kuuweka juu kabisa kwa utaratibu. Upeleke mpaka uhisi kuwa umefika mwisho. Kisha uteremshe mguu kwa utaratibu mpaka ufike sakafuni.

Baada ya hapo, uinue mguu wa kushoto kwa njia ile ile. Fanya zoezi hili kwa raundi kama tatu.

### MAZOEZI YA LUNGES

Unatakiwa kujishika kiuno. kisha piga magoti kwa mguu mmoja. Mguu wa pili ukanyage chini kama kawaida. Kisha inuka mpaka miguu yote miwili ilainike kabisa.

Fanya hivi kwa mara kumi kisha uibadilishe miguu. Fanya zoezi hili kwa mara ishirini kwa kila mguu kwa mizungumo mitatu.

### MAZOEZI YA KUPANDA NGAZI

Iwapo nyumba unayoishi ina ngazi, basi utaweza kulifanya zoezi hili na kuongeza nyama za paja.

Utahitaji mfuko au mkoba unaobebwa mgongoni, halafu weka kitu au vitu vizito kwenye ule mkoba na uubebe mgongo.

Panda na kushuka katika ngazi mara nyingi uwezavyo.

MAPISHI

Na Mary Geofrey



# Utamu wa chachandu ya pilipili

TUNDA la pilipili ni kiungo kinachompa mlaji hamu ya kula chakula.

Pilipili inaweza kuwekwa kwenye chakula chochote pale mlaji atakapopenda au kama chachandu ili kuongeza ladha na hamu ya mlo.

Maandalizi

Chukua karoti tatu kubwa, Pilipili hoho moja, vitunguu saumu vitatu, vitunguu maji vitano, tangawizi moja, majani ya giligiliani, ndimu na chumvi.

Weka mafuta kidogo sana, pilipili mbuzi au mwendo kasi tatu au utakavyopenda, nyanya tatu zilizoiva vizuri, pilipili ya unga vijiko viwili vikubwa vya chakula.





Pia weka Oyster sauce kikombe kimoja cha kahawa, nyanya, hoho, karoti, vitunguu maji, vitunguu saumu, tangawizi, majani ya giligiliani yachambue.

### NAMNA YA KUPIKA

Katakata vitunguu maji na nyanya weka bakuli tofauti, twanga vitunguu saumu na majani ya giligiliani, kwangua karoti pia katakata pilipili hoho.

Bandika mafuta jikoni yakipata moto, weka vitunguu maji koroga dakika mbili weka vitunguu saumu na giligiliani koroga tia tangawizi kisha hoho na karoti.

Acha kidogo ichemke, halafu weka nyanya iliyochanganywa na pilipili ya unga, kamulia ndimu kasha tia chumvi na funika mpaka nyanya iive vizuri.

Ikichemka kwa muda wa dakika tano baada ya kuweka pilipili, weka oyster sauce na acha ichemke kisha epua iache ipoe.

Ukiona imepoa iweke kwenye blenda isage vizuri na hapo pilipili yako itakua tayari kwa ajili ya kuliwa.

## MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**

# Fanya haya kupendezesha mandhari ya nyumba yako



UTENGENEZAJI wa mandhari na mazingira yanayozunguka nyumba ni jambo jema na linaloleta fahari katika maisha ya binadamu.

Utengenezaji huu unapaswa kuleta uzuri, mvuto, afya na ustawi wa jamii inayoizunguka, huku yakizingatia uhifadhi wa mazingira.

Unapaswa uhusishe pia kubadili na kuboresha sura na kontua za ardhi, uboreshaji miti na mimea, kuweka vitu na samani katika mandhari husika kwa ustadi kubwa.

Bustani au uwanja wa nje ya nyumba wa kupumzikia, varanda na sehemu ya kuegeshea gari kwa waliobarikiwa kumiliki ni miongoni mwa maeneo muhimu ya kuyaweka katika mvuto na yanayochangia kupendezesha mandhari ya nyumba.

Eneo lingine linalopaswa kutengenezwa vizuri katika nyumba kwa ajili ya kuiongezea mvuto ni njia zinazopishana ndani ya nyumba husika, taa za nje, upandaji wa miti, maua na vifaa vya kuoteshea maua.

Utengenezaji huo unapaswa kuanza katika hatua za awali wakati wa kusanifu mazingira ya nyumba kwa kufuata utaalam unaoendana na uhifadhi wa mazingira.

Kutengeneza mandhari ya makazi yanayotuzunguka kuna faida nyingi, ikiwamo kuweka mazingira katika hali ya kuvutia. Hii inasaidia pia kuleta harufu ya mvuto nyumbani inayochanganyika na hewa nzuri ya maua yanayokuwa yamepandwa katika nyumba.

Nyumba ambayo mazingira yake yametengenezwa katika mandhari nzuri hupendeza na kuonekana ya mvuto zaidi hata kama ni ya kawaida.

Mazingira ya makazi yanapotengenezwa katika mshikamano wa kiuzuri husababisha eneo zima lionekane katika uzuri wenye kuvutia zaidi lakini pia huwa ni alama inayotambulisha hata aina ya watu wanaoishi humo.

Pia mandhari ambayo imepangiliwa vizuri kuanzia miti, maua pamoja na nyasi huwa katika sifa nzuri ya kulifanya eneo husika kuwa na hali ya utulivu na starehe, mpangilio wa kila kitu kilichomo ndani huvutia nafsi ya mtu kupendelea kuwapo nyumbani.

Kwa kawaida watu hupendelea mandhari nzuri kuzunguka makazi yao na hata mtu ambaye si mpenzi wa kutengeneza, pindi anapofika katika mandhari iliyotengenezwa vizuri hujisikia vyema na mwingine hujifunza na kwenda kutengeneza kwake.

Mandhari na mpangilio mzuri wa vitu nje ya nyumba husaidia kupunguza joto la eneo husika.





## MPANGILIO

## Dondoo unapotaka bafu lako kuwa la kisasa

**1: Kioo**
Weka kioo sehemu ya ukuta ambacho utakitumia kujiangalia wakati unasafisha kinywa, meno au kunyoa ndevu.


**2: Bomba**
Ni muhimu kuweka bomba la maji ya mvua au sehemu ya kunawia uso. Bomba la kunawia uso liwe karibu na kioo.

**3: Jakuzi**
Kwa wale wenye uwezo, hakikisha unaweka jakuzi liwe dogo au kubwa ndani ya bafu kwa ajili ya kuogea.

**4: Enga ya taulo.**
Ni muhimu kuwa na enga maalum ya kuhifadhia taulo na nguo zingine bafuni kwa ajili ya kutunza usafi wa mwili.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2021
SMS - 0621 412 879
MSITAKE NIWAGONGEE HODI KUULIZA KERO ZENU TOENI KERO ZENU KAMA MNAVYOTOA NJE VIROBA MKIONA GARI LA TAKA...
AFADHALI UMEKUJA LABDA HUYU MAMA ATAACHA KUTUUZIA 'NGUMU KUMEZA'
TUME-LALAMIKA SANA!
USINIZINGUE... KWANI NILIPOKWAMBIA HATI YAKO CHAFU ULIELEWA NINI?
NILIELEWA MWANDIKO WANGU MBAYA...
AH! MWAKA WENU MNATEMBEA HUKU MNAVIMBA!
TUSIVIMBE HIYO VEPE...
WEEE! USIJIFANYE KUNIKOLEA KILA NINAPOKUFYONZA UTANIPONZA MWENZAKO MAMA HACHEZEWI..
HESHIMA BADO IPO PALE PALE...
ULIDHANI WALE WA 'UNANIJUA MIE NANI!' WATAREJEA?
WALISHAANZA ILA WAMEKU-TANA NA 'KIGINGI' WAMENYWEA!
HAITAPOTEA KIRAHISI KAMA SINDANO MCHANGANI
UONGO! WALIANZA WAPI?
DALA-DALA
'HAYA MABANGO' NITAYAEPUKA KWELI NISIPOJIPELEKESHA!
STORI ZA HUMU KILA SIKU KUNA MPYA
SAMTAIMU DALADALA KAMA BUNGE BILA SPIKA HA HAA!
USHANIPENDA TANGAZA NDOA
GARI LA MATANGAZO LINALIPIWA SHILINGI NGAPI?
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...MJINGA MKALIE KIMYA AJIPE USHINDI.

HABARI KIMATAIFA

# Hivi ndivyo atazikwa Prince Philip



**London,** Uingereza

WAKATI viongozi mbalimbali duniani wanaendelea kutoa salamu za rambirambi kwa Malikia Elizabeth wa Uingereza baada kifo cha mume wake Prince Philip (pichani), maandalizi ya mazishi yameanza rasmi.

Prince Philip, alifariki dunia siku ya Ijumaa akiwa na umri wa miaka 99, baada ya afya yake kuzorota kwa kipindi kirefu.

Hata hivyo maelezo ya maandalizi ya mazishi yatatangazwa hivi karibuni, lakini inatarajiwa kuwa hafla ya sherehe badala ya taratibu za kiserikali kufuata inayohusu kifo cha mtu kutoka familia ya kifalme.

**NI KIPI KITAKACHOFUATA?**

Tayari Serikali ya Uingereza imetangaza bendera ya muungano na bendera za mataifa mengine kupepea nusu mlingoti kwenye majengo yote,

bendera za muungano katika majengo ya kifalme ambapo Malkia hayuko kazini pia zitapeperushwa nusu mlingoti.

Aidha, bendera ya kifalme ambayo inawakilisha enzi kuu na uendelezaji wa kifalme, haitapeperushwa nusu mlingoti, lakini itapepea katika maeneo ambako Malkia yupo.

Aidha milio ya bunduki itasikika maeneo yote ya Uingereza na Gibraltar kwa mara 41 kwa raundi moja kila dakika kwa muda wa dakika 40.

Meli za kifalme 'Royal Navy' zilizopo baharini, pamoja na HMS Diamond na HMS Montrose pia itapiga saluti milio ya honi kama kutoa heshima kwa mtawala huyo, ambaye aliwahi kuwa askari wa majini wakati wa vita vya pili vya dunia.

Kwa heshima, vyama vikuu vya kisiasa nchini England, Scotland na Wales vimesimamisha kampeni za uchaguzi wa mwezi ujao.

Pia bunge litakaa kesho ili kutoa nafasi wabunge kutoa rambirambi zao.

**CORONA YAZUIA UMMA KUSHIRIKI**

Masharti ya kuzuia usambaaji wa virusi vya Corona kwa kuzia mikusanyiko, kuna hatari wengi kutohudhuria mazishi ya mwanamfalme huyo.

Wananchi wametakiwa kutohudhuria hafla zozote za mazishi kwa mujibu wa kanuni na ushauri wa Mamlaka ya Afya ya Umma.

Familia ya kifalme pia imewataka watu wasiache maua na ujumbe wa rambirambi katika makao ya kifalme.

Kwenye Tovuti ya Familia ya Kifalme, wananchi wametakiwa kutoa michango katika mashirika ya hisani badala ya kuweka maua kama kumkumbuka Prince Philip. Kitabu cha rambi rambi cha mtandaoni kimefunguliwa kwa umma kutoa pole zao.

Jalada ambalo liliwekwa nje ya makazi ya Malkia, Buckingham likitangaza kifo cha Prince Philip, baadaye liliondolewa kwa sababu ya wasiwasi kwamba ingevutia umati wa watu.

Prince Philip inaripotiwa aliomba mazishi yake yasiwe na mbwembwe, alitaka hafla ndogo ambayo mwili wake usitazamwe na umma.

Badala yake jeneza lake litakuwa katika Kasri la Windsor ili kutoa heshima na wakati huo mwili kulazwa ukiwa wazi ili kuagwa na umma.

Hadhi kama hiyo walipewa wanafamilia watatu wa kifalme, wa mwisho alikuwa Mama wa Malkia mwaka 2002.

Diana, Malkia wa Wales pia alipewa aina ya mazishi ya kifalme ya sherehe licha ya kuwa hakuwa tena na taji la Utukufu wa Kifalme.

**NANI ATAHUDHURIA MAZISHI?**

Utaratibu baada ya kifo cha mtawala huyo , iliyeitwa jina la Forth Bridge, maelfu ya watu wangetarajiwa kukusanyika jijini London na Windsor, na wengine hata wangepiga kambi kupata mahali pa kutazama gwaride la jeshi.

Mamia ya wanajeshi wangekuwa wamejipanga barabarani kwa heshima ya kiongozi huyo, pamoja na maelfu ya maofisa wa polisi kudhibiti waombolezaji.

Lakini kutokana na janga la Corona. waandaaji wamekuwa wakifanya kazi kulingana na hali ya dharura kuhofia kuvutia mikusanyiko ya watu.

Malkia sasa anafuata mabadiliko ya mipango ya mazishi kwa kuzingatia ushauri wa serikali na miongozo ya watu kujitenga siku ya mazishi. Inaaminika jeneza lake litapelekwa umbali mfupi kwenda St George's Chapel kwa ajili ya misa.

Hata hivyo, Prince Harry, anaweza kuhudhuria kulingana na Press Association. Mtawala huyo wa Sussex anaishi Marekani na Duchess wa Sussex na hajarudi Uingereza tangu ajiondoe kwenye majukumu ya kifalme mwaka jana.

Wafalme, malkia na wakuu wa kifalme huzikwa ndani ya kanisa la Royal Vault.

**BBC**

---

## Iran yazindua vinu vipya vya nyuklia

**TEHRAN,** Iran

IRAN imetangaza kuanza kutumia mitambo mipya ya kisasa inayoweza kurutubisha haraka madini ya Urani.

Hatua hiyo inaweza kuonekana kuwa ni ukiukaji mwingine wa makubaliano ya nyuklia ya mwaka 2015 kati ya nchi hiyo na mataifa yenye nguvu

Katika tukio lililorushwa moja moja na televisheni ya taifa, Rais Hassan Rouhani wa nchi hiyo, alifungua rasmi mitambo miwili ya kisasa iliyofungwa kwenye kituo cha kurutubisha madini ya Urani cha Natanz.

Hayo yanajiri wakati awamu ya kwanza ya mazungumzo ya wanadiploamsia wa ngazi ya juu wanaojaribu kunusuru mkataba huo wa nyuklia kukamilika juzi mjini Vienna kwa kila upande kueleza kwa tahadhari kile kilichofanikiwa.

Wawakilishi wa kila upande walisema kuna mafanikio fulani yalipatikana kwenye mazungumzo hayo ya siku tatu na wanatarajiwa kukutana tena wiki inayo.

**DW**

---

## Rais Guelleh ashinda mara ya tano

**DJIBOUTI CITY,** Djibouti

SERIKALI ya Djibouti imesema kiongozi wa muda mrefu wa nchi hiyo, Omar Guelleh, ameshinda kwa kishindo katika uchaguzi mkuu uliofanyika siku ya Ijumaa. Akinukuu matokeo ya awali ya uchaguzi huo, Waziri wa Mambo ya Ndani ya nchi hiyo, Mumin Ahmed, ameliwaambia waandishi habari kuwa Guelleh, alipata ushindi wa asilimia 98 dhidi ya mpinzani wake Zakaria Farah.

Ingawa matokeo rasmi yanatarajiwa kutangazwa jana, , Rais Guelleh, ametumia ukurasa wake wa Twitter kuwashukuru wapiga kura kwa imani waliyomuonyesha na ametoa wito wa kuendelea kufanya kazi pamoja. Mgombea wa upinzani, Zakaria Farah, ambaye alisitisha kampeni zake mapema kutokana na wasiwasi wa usalama hajazungumza chochote kuhusiana na taarifa hizo.

## MAKALA

# VYOMBO VYA HABARI NI TAA IMULIKAYO GIZANI



Na Magabilo Masambu

**Sheria au kanuni zozote zinazotungwa kuminya uhuru wa maoni pamoja na uhuru wa vyombo vya habari kutoa habari ni kinyume cha Katiba kwa sababu hatuwezi kutunga sheria zinazovunja Katiba ambayo ni sheria mama.**

NI ukweli usiopingika kwamba maovu mengi hutendeka gizani japo yako yanayotendeka waziwazi mchana kweupe. Hii ndo kusema kwamba wale wote wanaokusudia ama kutenda kabisa maovu hupenda giza zaidi kuliko mwanga.

Ndivyo ilivyo hata katika uendeshaji wa nchi. Nchi zetu hizi hatuna malaika wa kutuendeshea lazima tujiongoze wenyewe na kwa sababu sisi ni binadamu wenye upungufu, lazima tusiaminiane kiasi cha kudhani kwamba yeyote anayekuwa madarakani ni tofauti na wale wasio na madaraka, kwa maana ya tabia na mienendo.

Kwa jinsi hii, lazima kuwapo na vyombo mbalimbali vya kudhibiti mienendo yetu, ndiyo maana tunazo mahakama, polisi na mamlaka nyinginezo. Hii yote inathibitisha kwamba hatujawa wakamilifu wala watakatifu.

Kwa mujibu wa katiba yetu ya nchi pamoja na upungufu mwingi unaotajwa, haijaacha kutamka haki ya watu kupashana habari, ama kutoa habari ama kupokea habari. Ibara ya 8(2) inasema "Kila raia anayo haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbalimbali nchini na duniani kote, ambayo ni muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi na pia juu ya masuala muhimu kwa jamii."

Sasa hatuwezi kuzungumzia uhuru wa kupashana habari, bila kuzungumzia uhuru wa vyombo vya habari vyenyewe. Hii ina maana kwamba vyombo vya habari vinapaswa kuwa huru katika kutafuta, kutafiti na kutoa habari hasa zile ambazo zinahusu maslahi ya taifa na watu wake.

Vyombo vya habari ni taa imulikayo mazuri na mabaya ambayo yanafanywa na yeyote bila kubagua ili mradi aliyetenda ni mwananchi. Bahati mbaya sana tuliyo nayo binadamu ni kufikiri mtu akishakuwa kiongozi, hasa Afrika, basi anageuka na kuwa malaika, hivyo maovu yanabaki kwa wananchi wa kawaida pekee kuliko yale ya viongozi yanayoathiri uchumi, siasa na uongozi wa nchi.

Sheria au kanuni zozote zinazotungwa kuminya uhuru wa maoni pamoja na uhuru wa vyombo vya habari kutoa habari ni kinyume cha Katiba kwa sababu hatuwezi kutunga sheria zinazovunja Katiba ambayo ni sheria mama.

Kama kweli tunaipenda nchi hii, hatujipendi basi kuna haja ya kuzipitia upya sheria zilizotungwa kwa ajili ya kudhibiti uhuru wa kutoa maoni. Pia Sheria ya Magazeti ya mwaka 1976 pamoja na marekebisho yake, ambayo inampa mamlaka waziri akijisikia tu anafunga chombo cha habari.

Uhuru wa vyombo vya habari kuchunguza na kutoa habari kwa umma kuhusu masuala mbalimbali ya utendaji wa viongozi wa serikalini, unasaidia hatua za haraka kuchukuliwa kwa wakati kuliko kujificha kisha baadaye ndipo ukweli ujulikane. Ukweli una tabia ya kusubiri wakati! Unaweza kuuficha lakini wakati ukifika kila kitu kinakuwa wazi.

Taarifa ya CAG ni ushahidi tosha kwamba panapokosekana uhuru wa vyombo vya habari, basi taifa linaingia kwenye hasara kubwa na kunufaisha watu binafsi kuliko maslahi mapana ya taifa. Vyombo vya habari ni vyenzo muhimu katika kupambana na ufisadi na wizi ndani ya serikali. Viongozi hawana dhamana na mali za umma, kwa hiyo wanaokiuka maadili ya kazi ni muhimu kuwekwa hadharani bila kusubiri kwa sababu nchi hii ina watu wengi wenye sifa za kuwa katika nafasi hizo.

Wakati tukipigania uhuru wa nchi hii, moja ya vikwazo na ambavyo vilichelewesha uhuru wetu ni pamoja na sheria mbovu na kandamizi za kikoloni ambazo zilizuia hata watu kukusanyika na kuzungumza kuhusu nanma ya kujikomboa, tulivyopata uhuru, baadhi ya sheria hizo tukabaki nazo. Mfano makosa ya uchochezi ambapo kupitia sheria hizo Mwalimu Julius Nyerere, Rais wa Kwanza wa Tanzania, amewahi kushtakiwa nazo halafu leo karibu miaka 60 ya uhuru bado tunakumbatia sheria hizo.

Kuna umuhimu wa kubadilika sasa tuone ukosoaji ni sehemu tu ya maisha na kama tunaogopa kukosolewa basi tusiombe nafasi za uongozi. Kama hatutendi maovu tunaogopa nini?

Wako wengine wanasema tunavyo vyombo vya habari vingi ni kweli, lakini wingi wa vyombo vya habari hakiwezi kuwa kipimo sahihi cha uhuru wa habari. Tuwashe taa tuziweke katika mapaji yetu ya uso ili kuona vizuri gizani. Taarifa zinapokuwa wazi kwa wakati, ukosoaji utapungua kwa sababu hatuwezi kuzungumzia mambo yaliyo wazi bali yaliyojificha.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Msisimko Challenge Cup kama wa Kombe la Dunia



Na Adam Fungamwango

**Kombe la Challenge kwa Wabongo miaka hiyo lilikuwa maarufu zaidi kuliko hata Kombe la Dunia ambayo matokeo ya mechi yanakuja kujulikana siku tatu baada ya mechi kuchezwa kwa kutangazwa na RTD. Si kama hivi sasa ambapo inaonekana laivu kwenye televisheni mechi ya kwanza hadi fainali.**

KWA sasa limekosa mvuto na halina msisimko tena kama ilivyokuwa mwanzoni mwa miaka ya 1980, hadi katikati ya miaka ya 1990. Nalizungumzia Kombe la Challenge. Ni kombe linaloshirikisha timu za taifa kutoka nchi za Afrika Mashariki na Kati.

Kwa miaka ya karibuni lilionekana kubadilika na kuzishirikisha zaidi nchi za ukanda wa nchi wanachama wa Baraza la Vyama vya Soka Afrika mashariki na Kati (CECAFA) kukiwa pia ongezeko la nchi kama, Burundi, Rwanda, Sudan Kusini, Eritriea na nyinginezo.

Miaka ambayo Kombe la Challenge liliwateka mashabiki wa soka nchini vilivyo ilizishirikisha hizo nchi nilizozitaja mwanzo hazikuwapo na badala yake kulikuwa na nchi ambazo kwa sasa hazichezi kwenye michuano hiyo na hata kama ikitokea moja, basi itakuwa imeliakwa tu.

Nchi hizo ni Zambia, Malawi na Zimbabwe. Kombe hili lilianzishwa na lililokuwa Shirikisho la Vyama vya Soka Afrika Mashariki na Kati (sasa Baraza).

Hapa Tanzania michuano hiyo inapofanyika nchi yoyote ile, basi mashabiki wa soka walikuwa wanaifuatilia kupitia redio ya taifa, Radio Tanzania Dar es Salaam (RTD).

Iwe inafanyika nchini au nchi yoyote, mtangazaji au watangazaji wataambatana na timu kwenda kutangaza moja kwa moja michuano hiyo.

Na zilikuwa zinatangazwa mechi zote kwa sababu nchini hakukuwa na teknolojia ya televisheni au mitandao, Watanzania walikuwa wakiifuatilia kupitia redio zao tu.

Kombe la Challenge kwa Wabongo miaka hiyo lilikuwa maarufu zaidi kuliko hata Kombe la Dunia ambayo matokeo ya mechi yanakuja kujulikana siku tatu baada ya mechi kuchezwa kwa kutangazwa na RTD. Si kama hivi sasa ambapo inaonekana laivu kwenye televisheni mechi ya kwanza hadi fainali.

Kutokana na michuano hii kupendwa na kufuatiliwa sana na Watanzania wengi miaka hiyo, hadi leo hii kuna majina ya wachezaji wa timu za nchi zilizokuwa zinashiriki michuano hiyo hayatosahaulika. Si wote, bali wale walioku wa mahiri na mastaa sana wakati huo.

Ndiyo maana hadi leo Watanzania hawajawasahau wachezaji wa timu ya taifa ya Zambia waliofariki kwa ajali ya ndege Aprili 27, 1993 pwani ya Gabon walipokuwa wakienda kucheza mechi ya kusaka tiketi ya kucheza Kombe la Dunia dhidi ya Senegal.

Ni kwa sababu mwaka mmoja uliopita wakifika nchini Tanzania kucheza Kombe la Challenge na kufanya vema, ikiacha gumzo kubwa kutokana na kuwa na wachezaji mahiri. Ilishika nafasi ya tatu kwa kuifunga Malawi mabao 4-0, huku Uganda ikitwaa ubingwa kwa kukichapa kikosi cha pili cha Taifa Stars kilichojulikana kama Kakakuona bao 1-0.

Ndiyo maana Watanzania waliwalilia sana kina Efford Chabala, John Soko, Whiteson Changwe, Robert Watikayeni, Eston Mulenga, Derby Makinka, Moses Chikwalakwala, Wisdom Mumba Chansa, Kelvin Mutale, Numba Mwila, Patrick Banda, Kenan Simambe, Timothy Mwitwa, Richard Mwanza, Moses Masua na wengineo.

Timu ya taifa ya Zambia siku zote wapinzani wao wakubwa walikuwa na Malawi. Nao kwenye miaka ya 1980 hadi katikati ya 1990 walikuwa na wachezaji walioondokea kuwa maarufu.

Nao ni Jonathan Bilie, Jack Chamangwana, Young Chimodzi, Stocker Danzide, Clement Mkwalula, Jimmy Mfamba, Clifton Msiya, Frank Sinalo, Collin Thewe, Herman Malunga, Lawrence Waya na ndugu yake Harry Waya.

Timu ya taifa ya Zimbabwe ilikuwa na wachezaji kama Mosses Chunga, Shacky Tauro, Stanley Ndunduma, Oliver Kateya, Carlos Max (Mzungu), Madzimba Dinyero na wengineo.

Harambee Stars, timu ya taifa ya Kenya ilikuwa na wachezaji mahiri kama Mahmoud Abbas, Elly Adero, JJ Masiga, Peter Otieno Basanga, James Ouma, Josephat Murila, Nashon Mahila, Sammy Tabu, Bob Ogola, Hussein Kheri, Francis Kadenge, Ambroce Ayoyi na Wilbaforce Mulamba.

Uganda nayo haikuwa nyuma. ilikuwa na wachezaji wasiosahaulika kama Paul Hasule, Godfrey Katerega, Godfrey Higenyi, John Latigo, Fred Mukasa, Paul Nkata, Phillip Omondi, Issa Ssekatawa, Adam Ssemugabi, Majid Musisi na Jackson Mayanja.

# HADITHI

KWANI mapenzi ni nini? Si kumpenda yule unayemtaka wewe? Kwa nini inafika wakati watu wanapangiana? Je, ukilazimisha yanaitwa mapenzi? Si yatafanana na utumwa? Yeyote anayetaka kulifanya penzi liwe na matabaka, rangi, kabila, anaweza kusababisha maafa makubwa. Donald. Kijana msomi aliyetoka Marekani, anarejea Tanzania. Akakabidhiwa kuendesha kampuni za baba yake lakini pia anatakiwa aoe. Hapo ndipo tatizo linapoanza. Usikose hata nakala moja ya riwaya hii tamu na ya kusisimua.

# Sumu ya Mapenzi-1

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**




"WAPI hapo polisi?" Sauti iliita toka upande wa pili ya simu ya mezani.

"Ndiyo, nazungumza na nani?"

"Haina haja na kujua mimi ni nani?"

"Sasa kwa nini umepiga kama hutaki tujue wewe ni nani?"

"Lengo si hilo afande. Lengo ni kukufamisha tu kuwa kuna mzigo wako pale Sinza Afrika Sana."

"Mzigo gani?"

"Utaujua huko huko, kwa heri ya kuonana." Simu ilikatwa.

Inspekta Andrew aliutazama mkono wa simu kwa hasira kana kwamba ndiyo alikuwa anazungumza nao.

Mara nyingi hupata simu za wahuni kama hao ambao wanaona raha kuwapigia simu askari polisi na kuwaambia maneno ambayo wakati mwingine ni ya dhihaka na si ya kweli.

Namba za bure ambazo askari polisi wamezitoa kwa wateja wao mara nyingi hazitumiwi vizuri, badala yake kumekuwa na baadhi ya watu wanazichezea kwa kuleta mizaha na hata kuwatukana polisi.

Kwa sababu hawatarishi usalama wa nchi au watu wengine, polisi wamekuwa wakiacha tu. Utakamata wangapi kwenye nchi ambayo ina watu wenye akili tofauti.

Ndiyo maana wengine wanaweza hata kuchukua namba za askari wa zimamoto wanasema kuna mahala fulani jengo au nyumba inaungua. Lakini ukifika huko hawakuti kitu chochote.

Kuna baadhi ya watu ambao wao huona raha tu wenzao wakisumbukuka.

Inspekta Andrew aliingiwa na wasiwasi kidogo. Ni kweli hupokea simu za mizaha matusi na kila aina ya kejeli, lakini kwa askari mzoefu kama yeye, hata sauti za wapigaji zinaonyesha kuwa ni watu wa aina hiyo.

Sauti hii iliyoisikia punde haikuwa hivyo. Ilikuwa nzito na tulivu. Ilionekana kama mtu anayeongea kwa mamlaka fulani. Mtu aliyeongea alionekana kama ana uhakika na anachokiongea. Hakuongea maneno mengi.

Akaanza kupatwa na wasiwasi. Awali aliipuuzia simu hiyo ilipokuwa inapigwa. Hata ilipokatika ilipigwa tena.

Sauti ya mlio ilimkera na kuamua kuisikiliza ili mradi tu mpigaji asipige tena.

Ilikuwa zamu yake sasa. Alinyanyua mkono na kubonyeza namba kadhaa.

"Hapo, Sajenti Peter nakuomba ofisini mara moja." Alipomaliza alikata simu.

Dakika moja baadaye aliingia afande ambaye alikuwa amevaa sare. Akapiga saluti.

"Nenda kwenye kituo cha polisi kilicho karibu na Sinza Afrika Sana. Halafu baada ya hapo nendeni maeneo ya Sinza Afrika Sana mkafanye doria, huenda kuna kitu ambacho si cha kawaida."

"Sawa afande." Aliitikia afande Peter.

Alitaka kumuuliza bosi wake "Kwani umesikia kuna nini?" Lakini taratibu za kupolisi haziruhusu. Unachotakiwa ni kutimiza amri wa mkuu wako tu.

"Kuna mtu amenipigia simu, inauonekana kuna tatizo." Alimaliza Inspekta Andrew na kuchukua gazeti, akaanza kusoma.

Dakika tano baadaye aliliweka chini. gazeti halisomeki

"Kuna mzigo wako pale Sinza Afrika Sana." Sauti nzito ya mtu yule ilimjia tena kwenye ubongo wake.

Yeye kama polisi mzoefu, hakutegemea kuwa ni mzigo tu wa kawaida kama alivyosema, bali ni tatizo. Alinyanyua tena simu na kupiga Makao Makuu ya Kampuni ya simu na kuzungumza nao.

Alichotaka ni kujua siku ile ilipigwa wapi na ni nani.

Dakika kumi baadaye simu iliita mezani kwake. Aliiangalia kwa uchungu. Alidhani kuwa Sajenti Peter.

"Mkuu tunapenda kukufahamisha kuwa simu ile ilipigwa maeneo ya Posta, Dar es Salaam. Kwa bahati mbaya sana imepigwa na mteja kwenye kibanda cha simu." Simu ilipokatwa alicheka kicheko kifupi ambacho hakukuwa halisi. Hata mwenyewe hakujua ni cha nini.

> **"Mkuu tunapenda kukufahamisha kuwa simu ile ilipigwa maeneo ya Posta, Dar es Salaam. Kwa bahati mbaya sana imepigwa na mteja kwenye kibanda cha simu." Simu ilipokatwa alicheka kicheko kifupi ambacho hakukuwa halisi. Hata mwenyewe hakujua ni cha nini.**

Alichoambiwa alikitegemea. Hakuwa mmoja wa watu ambao wanapiga simu ovyo ovyo na kulisumbua Jeshi la Polisi. Huyu alikuwa anajua anachokifanya. Hakupiga simu ya mkononi. Na wala hakupiga simu kwa kutumia simu ya mezani ikiwa nyumbani. Alijua atapatikana. Na wala hakutaka kwenda kibanda cha simu ya mitaani. Aliamua kwenda Posta ambako kuna mkusanyiko wa watu wengi.

Kwa maana hiyo alitegemea kitu kibaya kutokea dakika si nyingi zijazo.

Simu iliita tena, akainyanyua mkono.

"Afande nipo kwenye eneo la tukio. Niko wa wenzangu wa kituo kidogo cha polisi cha jirani hapa. Ni kwamba maeneo ya Afrika Sana tumeukuta mtu amefariki dunia. Ni mwili wa mwanamke ambaye ana miaka kuanzia 23 hadi 26 hivi afande. Ulionekana alfariji kwenye mtaro. Kwa mujibu wa watu hapa wanadhani kwamba huenda ni mmoja wa wanawake makahaba na inawezekana amegongwa na gari au ameuawa. Hilo nadhani litajulikana baadaye uchunguzi utakapofanyika afande."

Ilikuwa ni taarifa fupi ya awali kutoka kwa afande Peter, lakini inayojitosheleza kwa wakati huo.

Inspekta Andrew mpaka wakati huo hakushangazwa na taarifa ya kuokotwa kwa maiti ya mwanamke. Alishaambiwa kuwa kuna zawadi yake na mtu huyo 'muuaji mjivuni'.

Yeye ameshatambua kuwa hayo ni mauaji. Ni kwa sababu ametaarifiwa na mtu aliyeonekana amefurahia kifo hicho. Kitu ambacho ameshangazwa kidogo ni jinsi msichana huyo alipotupwa kwenye mtaro na lengo lionekanane kama amegongwa na gari.

Isingekuwa sauti ya yule jamaa, inawezekana kila mmoja angejua huenda mwanamke huyo amegongwa na gari.

Ambacho kwa sasa anachosubiri ni taarifa tu ya madaktari ili kazi ianze na kufuatilia ni nani wamehusika kwenye mauaji hayo na pia kumfutilia mtu ayepiga simu kuitaarifu polisi juu ya mauaji hayo na anahusika vipi.

**ITAENDELEA JUMAPILI**



## UMEMALIZA MWENDO
# TUTAKUKUMBUKA DAIMA DMX

DUNIA inaendelea kuomboleza kifo cha rapa mashuhuri, Earl Simmons maarufu kama DMX, ambaye alifariki usiku wa kuamkia jana akiwa na umri wa miaka 50.

DMX amefariki katika Hospitali ya White Plains iliyopo jijini New York, Marekani, akipatiwa batibabu kutokana na kuzidisha dozi ya dawa ya kulevya.

Chanzo kimoja kimesema mwanamuziki huyo alipata mshuko wa moyo baada ya kuongeza kiwango cha matumizi ya dawa za kulevya akiwa nyumbani kwake na kukimbizwa hospitalini kunusuru maisha yake.

Rapa huyo alipewa kifungo cha miaka mitano, lakini aliachiliwa huru baada ya kutumikia kipindi cha miaka mitatu. Hata hivyo maisha yake yaliwaliwa na matumizi yaliyokithiri ya dawa hizo.

Watu watamkumbuka kwa nyimbo zake tamu kama 'Get at me dog', 'Ruff ryders anthem', 'Money power respect' na 'Party Up'. Katika upande wa uigizaji alicheza filamu kama 'Cradle 2 the grave', Belly, Never Die Alone, Beef, Beyond the law na nyinginezo.

## Lupita afurahia maisha Serengeti

MWIGIZAJI wa Hoollywood, Lupita Nyong'o ambaye ni raia wa Kenya, amefurahia mapumziko yake katika mbuga ya wanyama ya Serengeti, iliyoko Kaskazini ya Tanzania.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Lupita alichapisha picha akionekana yupo mbugani na kuandika ujumbe unaoashiria anafurahia likizo yake akiwa katika eneo hilo lililotajwa namba moja kwa kuvutia duniani.

Filamu ambazo ameshiriki kucheza ni Queen of Katwe mwaka 2016, Star Wars The Rise of Skywalker (2019), Little Monster (2019), Black Panther (2018) na US (2019)



## Diamond kuzoa Bilioni 11.5

MSANII maarufu wa muziki wa Bongo Fleva, Diamond Platnumz, amethibitisha kuweka saini mkataba wa Sh. Bil 11.5 na kampuni moja ya usambazaji muziki.

Kampuni hiyo inayofahamika kama Mziiki, itasimamia kazi zote za wasanii wanaomilikiwa na lebo ya Wasafi.

Kupitia mtandao wake wa kijamii wa instagram, Diamond ameandika ujumbe huo ambao utafanya lebo hiyo kuongoza Afrika Mashariki kwa utajiri.



# Pochettino: Mbappe atabaki PSG kwa muda mrefu

**PARIS,** Ufaransa

MAURICIO Pochettino ameahidi Paris Saint-Germain itapigana kwa nguvu zote kumbakiza, Kylian Mbappe wakati huu uvumi ukizagaa kwamba, nyota huyo wa Ufaransa anahusishwa na Real Madrid.

Kulikuwa na madai kwenye vyombo vya habari vya Hispania Alhamisi kwamba, Mbappe ameiambia PSG anataka kwenda Madrid mwishoni mwa msimu huu, klabu ambayo amekuwa akivutiwa nayo tangu akiwa mtoto.

Mbappe ambaye ni mshindi wa kombe la Dunia na Ufaransa, mkataba wake wa sasa unamalizika mwishoni mwa msimu ujao, lakini yeye ameripotiwa kutaka kuondoka kipindi kinachokuja cha majira ya joto.


Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 amekuwa muhimu kwa PSG, huku akitoka kufunga mabao mawili dhidi ya Bayern Munich kwenye mchezo wa kwanza wa robo fainali ya Ligi ya mabingwa Ulaya, wakati wakishinda 3-2.

Alipoulizwa kuhusu taarifa hizo, kocha wa PSG, Pochettino alisema: "Hiki ni kitu cha kawaida.

"Wakati tunapozungumza kuhusu klabu kubwa na wachezaji wakubwa kama Kylian Mbappe, ambaye ni mchezaji wa daraja la juu, uvumi mara zote utakuwapo.

"Kitu cha muhimu ni kwamba, Kylian Mbappe ametulia na akili yake ni kuisaidia timu kufikia mafanikio.

"Ni mchezaji aliyepevuka licha ya umri wake kuwa mdogo. Nimeshasema kwamba, klabu na chezaji wanajipanga kufikia makubaliano mapya na Kylian anaweza kubaki na sisi kwa muda mrefu sana."





# ZIDANE ANA MATUMAINI MESSI HATAONDOKA BARCELONA

**MADRID,** Hispania

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane, amesema ana matumaini, Lionel Messi atabakia Barcelona wakati huu uvumi ukienea kwamba, anataka kuondoka mwishoni mwa msimu huu.

Messi amekuwa akihusishwa na kutaka kuondoka Barcelona, huku akitajwa kuwa anaweza kwenda kuungana na kocha wake wa zamani, Pep Guardiola kule Manchester City.

Nyota huyo wa Argentina mwenye umri wa miaka 33 ametumia karibia muda wake wote wa kucheza pale Barcelona, ambako alijiunga nayo wakati akiwa kijana mdogo mwaka 2000.

"Matumaini yangu atabakia Barcelona," alisema Zidane, akizungumza kabla ya mchezo wa jana Jumamosi wa Clasico.

"Akiwa pale ni vizuri zaidi na vizuri kwa Ligi Kuu ya Hispania."

Mchezaji mwingine ambaye amekuwa akihusishwa na kuondoka mwishoni mwa msimu huu ni mlinzi wa Real Madrid, Sergio Ramos, ambaye mkataba wake unafikia mwisho.

Ramos aliukosa mchezo wa jana Jumamosi dhidi ya Barcelona kutokana na kuwa majeruhi.

# Guardiola hana tabu Aguero akibaki EPL

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola amesema kuwa hana tatizo na mshambuliaji wake, Sergio Aguero kama atajiunga na timu inayoshiriki Ligi Kuu England.

Aguero anaondoka katika kikosi cha Man City mwishoni mwa msimu huu wakati mkataba wake utakapokuwa umefikia mwisho na tayari mabosi wake wamekubaliana kwamba hawatamwongezea mkataba mpya.


Nyota huyo ambaye ni mfungaji bora wa wakati wote wa Man City akiwa amefunga jumla ya mabao 257, amekuwa akihusishwa kujiunga Chelsea na Manchester United ambazo zinampigia hesabu raia huyo wa Argentina mwenye umri wa miaka 32.

"Sisi wote tunamtakia kila la heri yeye, tutaheshimu uamuzi ambao ataamua, tunajua kwamba itakuwa ni bora kwake na familia pia," alisema Guardiola akinukuliwa na BT Sport.

"Tuna kazi ya kumtafuta Aguero mwingine tena, lakini kile ambacho atakiamua yeye sisi hatuna tatizo naye, kizuri kwake ni kizuri kwetu pia.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MANCHESTER UNITED YAMUWANIA OBLAK

## Wanapanga kumpa mikoba ya kumrithi De Gea, huku Henderson...

**MANCHESTER,** England

GOLIKIPA wa Atletico Madrid, Jan Oblak, ameripotiwa kuwaniwa na Manchester United ambao wamekuwa wakivutiwa na raia huyo wa Slovenia kwa muda mrefu, kwa mujibu wa 90min.com.

**Suala la kipa pale Man United limekuwa kizungumkuti kuelekea mwishoni mwa msimu huu.**

David de Gea amekuwa akihusishwa na mpango wa kutaka kuondoka pale Old Trafford, huku Dean Henderson bado hajaweza kutoa ushawishi wa kutosha ili kuwa golikipa namba moja.

Na sasa Man United wamekuwa kwenye windo la kutafuta golikipa mpya na mashetani wekundu hao wametoa jicho lao kwa Oblak pale Madrid.

Oblak ametumia miaka saba akiwa na Ateltico yenye maskani yake kwenye mji mkuu wa Hispania, Madrid, lakini yeye mwenyewe yupo tayari kwenda nchini England.

Kwa mujibu wa ripoti, Oblak amekuwa akivutiwa na Ligi Kuu ya England na sasa ana wakati mzuri zaidi wa kwenda huko.

Ripoti zaidi kwamba, United wanashaka kuhusu Henderson kuwa kipa namba moja na sasa wanapanga kumchukua Oblak mwenye umri wa miaka 28.

## ZISIKUPITE

### CAVANI HAJUI HATIMA

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer amesema straika wa Uruguay, Edinson Cavani mwenye umri wa miaka 34, bado hana uhakika kama atabakia klabuni hapo mwishoni mwa msimu huu. ***(Manchester Evening News)***

### SPURS WAMTAKA KOKCU

KLABU yaTottenham Hotspur inamuwania kiungo wa Feyenoord na Uturuki, Orkun Kokcu, mwenye umri wa miaka 20, lakini inakabiliwa na ushindani kutoka kwa Arsenal. ***(Mail)***

### KONATE ANAWEZA KUTUA LIVER

LIVERPOOL inaweza kumsajili mlinzi wa RB Leipzig na Ufaransa, Ibrahima Konate mwenye umri wa miaka 21, kwa chini ya euro milioni 40. ***(Bild journalist Christian Falk)***

### VESTERGAARD KUBAKI

KLABU ya Southampton "itafanya kila kitu" kumbakiza mlinzi wake wa kati raia wa Denmark, Jannik Vestergaard mwenye umri wa miaka 28, amesema kocha wa klabu hiyo, Ralph Hasenhuttl kujibu uvumi wa kuwawa Tottenham. ***(Daily Echo)***

### AANHOLT APEWA MIAKA 3

MLINZI wa Crystal Palace, Patrick van Aanholt mwenye umri wa miaka 30, amepewa ofa ya mkataba wa miaka mitatu na Galatasaray. Raia huyo wa Uholanzi mkataba wake wa sasa unamalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Sky Sports)***

### LIVERPOOL KUMSAJILI KOBAK

LIVERPOOL ipo tayari kumnunua Ozan Kabak baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 raia wa Uturuki kuonesha kiwango cha kuvutia kule Schalke anakocheza kwa mkopo. ***(90min)***

### GUARDIOLA NA AGUERO

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amesema hatakuwa na tatizo kama mshambuliaji wake, Sergio Aguero mwenye umri wa miaka 32, atajiunga na klabu yoyote kwenye Ligi Kuu ya England, wakati atakapoondoka pale Etihad mwishoni mwa msimu huu. ***(Sun)***

### ICARDI KUONDOKA PSG

STRAIKA wa Argentina, Mauro Icardi, 28, anangalia uwezekano wa kuondoka Paris St-Germain kipindi cha majira ya joto kinachokuja. ***(L'Equipe)***

### SPURS YAMTAKA JOHNSTONE

TOTTENHAM Hotspur inaongoza kwenye mbio za kuwania kumsajili golikipa wa West Bromwich Albion, Sam Johnstone mwenye umri wa miaka 28. ***(ESPN)***

### PALACE WAMUWINDA HOWE

KLABU ya Crystal Palace inataka Eddie Howe achukua mikoba ya kocha, Roy Hodgson baada ya bosi wa zamani wa Bournemouth kubadilisha uamuzi wake na kujiunga na Celtic. ***(Football Insider)***

HABARI MICHEZO

# AZAM FC YAIENGUA SIMBA, YALIPA KISASI

**Na Adam Fungamwango**

MABAO mawili yaliyofungwa na Mzimbabwe Prince Dube, yameifanya timu ya Azam kuiengua Simba kileleni, ikishinda 2-0 dhidi ya Mtibwa Sugar kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

**Ni ushindi ambao pia umeifanya Azam kulipa kisasi cha kufungwa bao 1-0 kwenye mechi ya mzunguko wa kwanza.**

Ushindi huo unaipeleka Azam hadi nafasi ya pili ambayo kwa muda mrefu ilikuwa inakaliwa na Mabingwa Watetezi Simba, ambao hawajacheza mechi nyingi kutokana na majukumu ya kuiwakilisha nchi kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika.

Azam imefikisha pointi 47 kutokana na mechi 25 ambazo imecheza, hata hivyo imeizidi Simba pointi moja tu.

Simba ina pointi 46, lakini imecheza mechi 20 na hii ina maana kuwa Azam imecheza mechi tano zaidi ya Simba.

Wanalambalamba hao wanaonekana kurudi kwenye hali yao ya kawaida, baada ya kupotea mwishoni mwa mechi za raundi ya kwanza.

Awali wakati Ligi Kuu Tanzania Bara inaanza Azam ilishinda mechi saba mfululizo na kuongoza kwa muda mrefu, kabla ya kufungwa na Mtibwa Sugar Oktoba 26, mwaka jana kwenye Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro.

Ni kipigo ambacho kiliifanya timu hiyo kuanza kupoteza mwelekeo na kuenguliwa kileleni na Yanga, lakini pia ikashindwa kukaa kwenye nafasi ya pili, badala yake kutupwa nafasi ya tatu ambayo ilikaa kwa muda mrefu.

Hata hivyo, inaonekana ni suala la muda tu, kwani viporo vitano vya Simba vinaweza kubadilisha sura nzima ya mwenendo wa ligi na nafasi ya Azam kwenye msimamo wa ligi kwa ujumla.



Bondia Twaha Kiduku wa Tanzania (kushoto), akipambana na mpinzani wake, Tshibangu Kayembe, kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, katika pambano lililofanyika Jumamosi usiku jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ihefu FC yachekelea sare

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Namungo FC kwenye Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa, mkoani Lindi, Kocha Mkuu wa Ihefu FC, Zuberi Katwila, ameleeza kufurahishwa na sare hiyo.

Akizungumza baada ya mechi hiyo iliyochezwa juzi, Katwila alisema kuwa mechi ilikuwa ngumu, hivyo vijana wake walijitahidi kwa hali na mali hadi kufanikisha sare hiyo.

"Tulitarajia kabisa kuwa mechi itakuwa ngumu, lakini kwa sare hii kwetu ni muhimu," alisema Katwila mchezaji wa zamani wa Mtibwa na pia kuwahi kuwa kocha wa timu hiyo.

"Kucheza na Namungo kwa sasa si jambo rahisi. Na sababu kubwa ni kwamba sisi tulikuwa mapumziko na wenzetu walikuwa wanacheza mechi za kimataifa, halafu wako kwao, si kitu rahisi."

Hata hivyo, Katwila alisema kuwa bado wana kazi kubwa kuhakikisha kuwa wanaondoka kwenye eneo hatarishi la kushuka daraja, hivyo wanahitaji ushindi kwenye mechi zinazokuja ili kujiweka salama.

"Pamoja na sare hii lakini hatupo salama. Salama yetu ni pale tu tutakaposhinda mechi zetu zinazofuata na kuangalia pia matokeo ya timu zingine," alisema.

Kwenye mechi hiyo, Ihefu ndiyo ilikuwa ya kwanza kupata bao lililofungwa na mchezaji wa zamani wa Yanga, Rafael Daudi, dakika ya 23, lakini Ibrahim Koko aliisawazishia Namungo bao dakika ya 61.

Ni matokeo ambayo yanaiweka Ihefu kwenye nafasi ya 17, ikiwa na pointi 21 kwa mechi 25 ambazo imecheza mpaka sasa.

Kwa upande wa Namungo, yenyewe inashika nafasi ya 10 kwa pointi 28 ilizonazo, lakini ikicheza michezo 18 tu mpaka sasa.

## Namungo yaikamia Nkana leo

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Namungo FC, Hemed Morocco amesema wanaenda kulipa kisasi dhidi ya Nkana FC katika kwenye mchezo wa marudiano wa hatua ya makundi kombe la Shirikisho Barani Afrika.

Mchezo huo utakaopigwa leo katika ardhi ya Ndola nchini Zambia huku Namungo wanashuka dimbani wakiwa na kumbukumbu za kufungwa bao 1-0, wiki iliyopita uwanja wa Benjamini Mkapa, jijini Dar es Salaam.

Akizungunza na gazeti hili, Morocco alisema wamejiandaa vizuri na wachezaji wako tayari kwa ajili ya kutafuta matokeo chanya.

Alisema walipoteza mechi ya awali na sasa wamejipanga kwa ajili ya kulipa kisasi kwa wapinzani wao hao kuhakikisha wanapata matokeo chanya.

"Tumejipanga vizuri wachezaji wana molari na tulipoteza nyumbani ila nina matumaini ya kwenda kupambana kutafuta matokeo ugenini," alisema Morocco.

Alisema watawakosa nyota wawili katika mchezo huo pamoja na Abdulhalim Humud ambaye ana tatizo la passport na Styve Nzigamasabo ambaye anatumikia adhabu ya kadi 3 za njano.

Baada ya mchezo wa leo Kikosi cha Namungo kimebakiza michezo miwili, watarejea nyumbani kuwakaribisha Raja Casablanca Aprili 21, uwanja wa Benjamini Mkapa.

## Kiduku: Kayembe alikuwa mgumu

**Na Mwandishi Wetu**

BONDIA Twaha Kiduku amesema pambano lake na mpinzani wake, Tshibangu Kayembe kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), lilikuwa zuri.

Katika pambano hilo la raundi nane lililofanyika kwenye ukumbi wa Ubungo Plaza Jumamosi usiku, Kiduku alishinda kwa pointi baada ya majaji watatu wa pambano hilo wote kumpa ushindi wa raundi 6 kati ya raundi 8.

Mara baada ta pambano hilo Kiduku alisema mpizani wake alijiandaa na ndio maana alishindwa kumpiga kwa KO na kwamba, pambano lilikuwa zuri.

"Pambano lilikuwa zuri, namshukuru Mungu kwa sababu mpinzani wangu naye alijiandaa," alisema Kiduku.

"Hii ni boxing huwezi kulazimisha kupata KO, nilijaribu lakini KO huja wakati wa mchezo ukiilazimisha utapata madhara," aliongeza kusema,

Twaha alionekana akiwa tofauti katika pambano hilo, akiwa ametulia na kupiga kwa kutafuta alama za ushindi zaidi kuliko mtindo wake uliozoeleka wa kutumia nguvu zaidi.

Kayembe ambaye aliwahi kupigana na Hassan Mwakinyo na kupoteza pambano hilo, alikuwa bondia mgumu dhidi ya Twaha katika pambano hili, akionesha uwezo wa kuvumilia masumbwi mazito.

# Michezo

Jumapili Aprili 11, 2021

Nipashe




Man United yamwania Oblak UKURASA 22



Beki wa kulia wa Simba, Shomari Kapombe, akijaribu kumtoka machezaji wa Al Ahly, Taher Mohamed, kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyochezwa juzi kwenye Uwanja wa Al Salam jijini Cairo. Simba ilifungwa 1-0, lakini ikiwa imefuzu hatua ya robo fainali, ikiongoza pia kundi A kwa pointi 13, Al Ahly, Mabingwa Watetezi wakishika nafasi ya pili kwa pointi 11. **PICHA NA MTANDAO**

## Mwambusi hana hofu na Simba

**Na Saada Akida**

KAIMU Kocha Mkuu wa Yanga, Juma Mwambusi, amesema hana hofu juu ya wapinzani wao Simba, katika mbio za ubingwa kutokana na uimara wa kikosi chao kwa ajili ya kutafuta matokeo chanya katika michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mwambusi alisema matumaini na malengo yao makubwa ni kupambana kupata matokeo mazuri katika kila mechi za ligi hiyo.

Alisema licha ya kuwapo kwa maneno mengi, amewaanda kisaikolojia na kiufundi wachezaji wake kwa ajili ya kupambana kutafuta matokeo chanya ili kufikia malengo yao.

"Yanga iko imara na mipango na malengo yetu ni kupambania mbio za ubingwa wa ligi hiyo, hatuwaangalii wapinzani wetu wanafanya nini, kikubwa kuhakikisha tunashinda mechi zetu tu," alisema Mwambusi.

"Hatuwapi nafasi maneno ya nje, tunawaandaa kisaikolojia wachezaji wetu, kila mmoja anatakiwa kufanya majukumu lake ikiwamo kufanya kazi vizuri wanapokuwa uwanjani," aliongeza.

Alisema ana matumaini makubwa ya kufanya vizuri na wako katika mbio za ubingwa msimu huu kwa sababu wanaongoza ligi hiyo.

"Kwanza tunaongoza ligi, pia ligi bado kuna mechi 10 hivyo kuna kila sababu ya kufanya vizuri katika mapambano ya ubingwa," alisema.

**Wakati huo huo**, Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli alisema wamepokea barua kutoka Shirikisho la Soka Tanzania, (TFF) kuwataka kesho Jumatatu kufanya kikao kuhusu suala la makamu Mwenyekiti wao, Frederick Mwakalebela.

# Chama: Nguvu zote robo fainali

### ●●● Asema sasa wanajiamini wanaweza kucheza na kupata ushindi kwa timu yoyote...

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuchapwa bao 1-0 dhidi ya Mabingwa Watetezi wa Afrika, Al Ahly ya Misri, klabu ya Simba imesema kuwa nguvu zake zote sasa inazielekeza kwenye mechi ya robo fainali ambako inaamini kuwa itafanya vizuri.

**Akizungumza mara baada ya mechi hiyo ya Kundi A ya Lig ya Mabingwa Afrika, mchezaji mwandamizi wa timu hiyo, Clatous Chama amesema kuwa amefurahishwa na kandanda safi ambalo yeye na wachezaji wenzake wamelionyesha na hii inawapa kiburi cha kutoihofia timu yoyote ile kwenye hatua hiyo.**

"Tulicheza vema sana. Tulikuwa na mchezo mzuri dhidi ya wapinzani wetu ambao ni wababe kwenye bara hili la Afrika. Na kwa sababu hiyo naamini mechi hii imetuongezea nguvu, ari na kujiamini." Alisema Chama.

Aliongeza; "Tumeona kuwa tunaweza sasa kucheza na kupata ushindi kwa timu yoyote ile tutakayokutana nayo, iwe nyumbani au ugenini."

Ikiwa ugenini kwenye Uwanja wa Al Salam jijini Cairo nchini Misri juzi Jumamosi usiku, Simba ilifungwa bao 1-0 na mabingwa hao wa kihistoria barani Afrika, kwa bao la Mohamed Sherif dakika ya 32.

Wakati Al Ahly ikicheza vema kipindi cha kwanza, Simba ilitawala mechi hiyo kipindi cha pili, hasa kuanzia dakika ya 60 hadi mechi ilipomalizika.

Al Ahly imelipa kisasi cha kufungwa bao 1-0 kwenye mechi ya kwanza Februari 23 mwaka huu, bao hilo likifungwa na Luis Miquissone kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, jijini Dar es salaam.

Simba ambayo imeonekana kuimarika msimu huu tofauti na mechi ya Februari 2, 2019 ilipochapwa mabao 5-0 nchini humo, iliwaweka wenyeji wake roho juu hadi mwamuzi alipopuliza filimbi ya kumaliza mechi.

Ni mechi ambayo Simba imepoteza kwa mara ya kwanza kwenye hatua hiyo ya makundi.

Hata hivyo, mechi hiyo haikuzidisha wala kupunguza lolote, kwani Simba imemaliza Kundi A ikiwa inaongoza kwa pointi 13, ikicheza mechi sita, kushinda nne, sare moja, ikipoteza mechi moja, mabao tisa ya kufunga, ikiruhusu mabao mawili tu.

Mabingwa Al Ahly, wanashika nafasi ya pili wakiwa wamemaliza mechi zao sita kwa pointi 11, ikishinda mechi tatu, sare mbili na kupoteza mechi moja ambayo ni dhidi ya Simba.

Hii ina maana kuwa timu hizo zimefungana zenyewe kwa zenyewe tu, kila timu ikishinda nyumbani wake.

Kwa sasa Simba inasubiri moja kati ya timu itakayoshika nafasi ya pili kwenye Kundi B, C na D, huku Al Ahly ikisubiri mshindi wa kwanza kwenye makundi hayo.


9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042